

MUHTASARI WA RIPOTI YA DUNIA YA UFUATILIAJI WA ELIMU

2024/5

# Uongozi katika elimu

## ONGOZA KWA AJILI YA ELIMU

unesco

Sustainable Development Goals

Global Education Monitoring Report

MUHTASARI WA RIPOTI YA DUNIA YA UFUATILIAJI WA ELIMU

**2024/5**

# Uongozi katika elimu

ONGOZA KWA AJILI YA ELIMU

Azimio la Incheon la elimu la 2030 na Mfumo wa Utekelezaji zinabainisha kuwa wajibu wa *Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu* ni kuwa "utaratibu wa kufuatilia na kuripoti juu ya Lengo nambari 4 katika Maendeleao Endelevu (SDG 4) na juu ya elimu katika malengo mengine". Wajibu wake ni "kuripoti kuhusu utekelezaji wa mikakati ya kitaifa na kimataifa ili kuhakikisha kuwa washirika wote husika wanatimiza ahadi zao kama sehemu ya ufuatiliaji na ukaguzi wa jumla wa malengo ya SDG". Ripoti hii imeandaliwa na timu ya kujitegemea kwa ushirikiano na UNESCO.

Majina yaliyotumika na uwasilishaji wa maudhui katika chapisho hili hayawasilishi maoni yoyote ya UNESCO kuhusiana na sheria ya nchi, taifa, jiji au eneo lolote lile, au mamlaka yake, au kuhusiana na uwekaji mipaka yake.

Timu ya *Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu* inawajibika kwa uchaguzi na uwasilishaji wa ukweli na maoni yaliyo katika kitabu hiki, ambayo si lazima yawe yanaambatana na yale ya UNESCO wala ya wafadhili wake na UNESCO haiwajibiki. Mkurugenzi wa timu hiyo anawajibika kwa mawazo na maoni yaliyotolewa katika Ripoti hii.


**_Timu ya Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu_**

*Mkurugenzi: Manos Antoninis*

Samaher Al Hadheri, Daniel April, Marcela Barrios Rivera, Madeleine Barry, Yekaterina Baskakova, Yasmine Bekkouche, Catarina Cerqueira, Rafaela Maria Da Silva Santos, Anna Cristina D'Addio, Dmitri Davydov, Francesca Endrizzi, Pablo Fraser, Lara Gil Benito, Pierre Gouëdard, Chandni Jain, Priyadarshani Joshi, Maria-Rafaela Kaldi, Josephine Kiyenje, Jodi Klue, Camila Lima De Moraes, Kate Linkins, Kassiani Lythrangomitis, Anissa Mechtar, Claudine Mukizwa, Yuki Murakami, Judith Randrianatoavina, Kate Redman, Maria Rojnov, Amina Sabour, Divya Sharma, Laura Stipanovic, Aziah-Katiana Tan na Dorothy Wang.



Ripoti ya *Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu* ni chapisho huru linalotolewa kila mwaka. Ripoti ya GEM imegharamiwa na muungano wa serikali mbalimbali, taasisi za kimataifa na mifuko binafsi na kuwezeshwa na UNESCO.

Ripoti hii inapatikana kwa kila mtu chini ya leseni ya IGO (CC-BY-SA 3.0 IGO) ya Attribution-ShareAlike 3.0 (http://creativecommons.org/licenses/by-sa/3.0/igo/). Kwa kutumia maudhui yaliyo ndani ya ripoti hii, watumiaji wanakubali kutii masharti ya matumizi ya UNESCO Open Access Repository (https://www.unesco.org/en/open-access/cc-sa).

Leseni ya sasa inasimamia sehemu ya maandishi pekee. Ili kutumia nyenzo yoyote ambayo haijabainishwa kuwa inamilikiwa na UNESCO, anayetaka kutumia atahitaji kuomba ruhusa mapema kutoka: publication.copyright@unesco.org au UNESCO Publishing, 7, place de Fontenoy, 75352 Paris 07 SP Ufaransa.

Leseni ya sasa inasimamia sehemu ya maandishi pekee. Ili kutumia picha, unahitaji kuomba ruhusa mapema.

UNESCO ni Mchapishaji Huru na machapisho yote yanapatikana mtandaoni, bila malipo kupitia hazina ya hati ya UNESCO. Mauzo yoyote ya machapisho yanayofanywa na UNESCO ni kwa ajili ya kulipia gharama ya uchapishaji au unakili wa maudhui haya kwenye karatasi au kanda za CD, na usambazaji. Lengo si kupata faida.

CC BY SA

Kichwa asili kwa Kiingereza: *Global Education Monitoring Report* Summary 2024/5 – *Leadership in education: Lead for learning.* Paris, UNESCO.

Ripoti hii inaweza kutajwa kama: UNESCO. 2024. *Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu 2024/5 – Uongozi katika elimu: Ongoza kwa ajili ya elimu*. Paris, UNESCO.

**Kwa taarifa zaidi, tafadhali wasiliana na:**
Timu ya Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu
UNESCO, 7, place de Fontenoy
75352 Paris 07 SP, Ufaransa
Barua pepe: gemreport@unesco.org
Simu: +33 1 45 68 07 41
www.unesco.org/gem-report

Makosa yoyote ya
kiuchapishaji au kuondolewa kwa baadhi ya maneno kwenye toleo litakalowekwa kwenye tovuti ya www.unesco.org/gemreport

© UNESCO, 2024
Haki zote zimehifadhiwa
Toleo la kwanza
Lilichapishwa 2024 na Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni

7, Place de Fontenoy, 75352
Paris 07 SP, Ufaransa

Mpangilio wa uchapishaji umefanywa na UNESCO
Mpangilio umefanywa na Apricot Business Solutions

Nukuu: Tarehe 3 Machi 2022 katika Shule ya Al Tasneem School huko Basra, Iraq, mkuu wa shule Ansal anasimama kupigwa picha katika ofisi yake. Anasema kwamba,"Umaskini, afya ya akili, ajira ya watoto, ndoa za watoto, ni baadhi masuala makuu kwa wanafunzi wetu … Umasikini ndilo tatizo kuu linalowafanya waache shule".

Picha: © UNICEF/UN0614639/Ibarra Sánchez*

https://doi.org/10.54676/FHWV5790
ED/GEMR/MRT/2024/S1

**Msururu wa Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu**

| | |
|---|---|
| 2024/5 | *Uongozi katika elimu: Ongoza kwa ajili ya elimu* |
| 2023 | *Teknolojia katika elimu: Nyenzo inayotumika kwa masharti ya nani?* |
| 2021/2 | *Wahusika wasio wa serikali katika elimu: Ni nani anayechagua? Ni nani anayepoteza?* |
| 2020 | *Ujumuishaji na elimu: Tukisema wote, basi ni wote* |
| 2019 | *Uhamiaji, ufurushwaji na elimu: Kuunganisha jamii badala ya kuigawanya* |
| 2017/8 | *Uwajibikaji katika elimu: Kutimiza ahadi zetu* |
| 2016 | *Elimu kwa ajili ya watu na dunia: Kujenga hatima endelevu kwa wote* |

**Msururu wa EFA wa Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu**

| | |
|---|---|
| 2015 | *Elimu kwa Wote 2000-2015: Mafanikio na changamoto* |
| 2013/4 | *Kufundisha na kujifunza: Kufanikisha ubora kwa wote* |
| 2012 | *Vijana na Stadi: Kufanya elimu yenye manufaa kwa kazi* |
| 2011 | *Mgogoro uliofichika: Mapambano ya silaha na elimu* |
| 2010 | *Kuzifika jamii zilizoko pembezoni* |
| 2009 | *Kuushinda ubaguzi: Umuhimu wa utawala bora* |
| 2008 | *Elimu kwa Wote kufikia 2015: Je, tutaweza?* |
| 2007 | *Msingi Imara: Malezi na elimu ya awali* |
| 2006 | *Kusoma, kuandika na kuhesabu kwa ajili ya maisha* |
| 2005 | *Elimu kwa Wote: Ubora ni kigezo* |
| 2003/4 | *Jinsia na Elimu kwa Wote: Kuelekea usawa* |
| 2002 | *Elimu kwa Wote: Je, dunia inafuata mwelekeo sahihi?* |

Ripoti hii na maudhui yote yanayohusiana yanaweza kupakuliwa hapa: http://bit.ly/2024gemreport

# UJUMBE MUHIMU

## Viongozi wa elimu ni zaidi ya wasimamizi. Wao ni wachochezi wa mabadiliko.

- **Watunga sera wanakabiliwa na changamoto kubwa:** jinsi ya kuhakikisha kwamba watu ambao wana ujuzi na maono yanayofaa wanatambuliwa, kuchaguliwa, kutayarishwa na kuungwa mkono kama viongozi.
- **Mipango ya kitaifa katika ngazi za shule, mifumo na za kisiasa inahitaji kukuza vipengele vinne muhimu vya uongozi:** kubainisha matarajio, kuzingatia masomo, kuhimiza ushirikiano na kuendeleza watu. Hata hivyo, uchambuzi wa kimataifa wa mipango na kozi za kuwatayarisha na kuwafunza wakuu wa shule ulidokeza kuwa ni kama nusu tu huzingatia kipengele chochote kati ya hivi vinne - na ni theluthi moja tu huzingatia vyote vinne.

## Shule bora zinahitaji viongozi bora wa shule.

- **Wakuu hodari wa shule huwapa wanafunzi motisha ya kupata matokeo bora zaidi.** Nchini Marekani, ilikadiriwa kuwa uongozi wa wakuu wa shule na walimu ulichangia hadi asilimia 27 ya tofauti katika matokeo ya wanafunzi; hii ni chini kidogo tu ya athari ya walimu kwenye mafunzo miongoni mwa vigezo vilivyosawazishwa kwenye shule.
- **Wakuu hodari wa shule huwapa walimu motisha ya kupata matokeo bora zaidi.** Utafiti uliofanywa katika nchi 32 ulidhihirisha kwamba uongozi bora unawiana na mbinu bora za ufundishaji. Duniani kote, asilimia 57 ya nchi zinatarajia wakuu wa shule watoe maoni kwa walimu kulingana na jinsi wanavyoona hali. Hata hivyo, sehemu ya wakuu wa shule za sekondari wanaosimamia shughuli za ufundishaji ilipungua kutoka asilimia 81 katika mwaka 2015 hadi asilimia 77 katika mwaka wa 2022 katika nchi zenye mapato ya juu.
- **Wakuu hodari wa shule huhakikisha kwamba shule zao ni salama, zina mazingira yenye afya na zinawajumuisha wote.** Kuzuia uonevu na kuhakikisha usalama wa wanafunzi ni malengo muhimu kwa viongozi wa shule. Nchini Marekani, wakuu wa shule walirekebisha mtalaa ili kupatia kipaumbele ustawi wa kijamii na kihisia wakati wa janga la COVID-19. Huko Malta, wakuu wa shule walishirikiana na jamii mbalimbali kukuza desturi za shule zinazowajumuisha wahamiaji kwa kutoa usaidizi wa lugha.

## Viongozi bora husisitiza haki katika michakato ya kuajiri, uaminifu na nafasi za kujiendeleza.

- **Michakato ya ajira yenye uwazi na ushindani inahitajika ili kupata na kudumisha wafanyakazi.** Kuwekea mipaka uhuru wa wanasiasa katika uteuzi wa wakuu wa shule huimarisha matokeo ya shule. Hata hivyo, ni asilimia 63 tu ya nchi ambazo zina michakato wazi na yenye ushindani ya kuajiri wakuu wa shule katika elimu ya msingi na ya sekondari.
- **Si kila wakati walimu bora huwa wakuu bora wa shule.** Ijapokuwa asilimia 76 ya nchi zimeweka sharti kwamba wakuu wa shule wawe walimu waliohitimu kikamilifu, nchi 3 kati ya kila 10 pia hubainisha wawe na tajiriba ya usimamizi.
- **Uhuru wa kufanya maamuzi unaweza kumsaidia kiongozi kufanikiwa.** Mifumo ya elimu inayopata matokeo bora zaidi sanasana huwapa wakuu wa shule uhuru zaidi wa kufanya maamuzi juu ya rasilimali watu na za kifedha. Lakini katika nchi zilizostawi zaidi, chini ya nusu ya wakuu wa shule wana wajibu juu ya maudhui ya masomo au kubaini kiwango cha mishahara ya walimu. Na karibu asilimia 40 ya nchi hazitambui uhuru wa taasisi za elimu ya juu kisheria.
- **Viongozi wataalamu wanahitaji maandalizi na mafunzo.** Kuweka viwango vya uongozi wa shule kunaweza kusaidia kuelekeza mafunzo kwa kubaini ujuzi unaohitajika; karibu nchi zote zimeweka viwango hivi. Hata hivyo, karibu nusu ya wakuu wa shule katika nchi zilizostawi zaidi hawakupokea mafunzo yoyote kabla ya kuteuliwa na ni asilimia 31 tu ya nchi zote ambazo zina kanuni za uelekezaji wa wakuu wapya wa shule wanapochukua hatamu. Ujuzi wa kiutendaji kama vile matumizi ya data, usimamizi wa fedha na ujuzi dijitali ni muhimu sana, hata hivyo, robo ya wakuu wa shule katika nchi zilizostawi zaidi hawajapata mafunzo ya kutosha ya masuala hayo.

## Viongozi wa shule hutarajiwa kufanya mengi sana kwa rasilimali chache mno.

- **Mahitaji ya uendeshaji wa shule ni mengi mno kiasi kwamba hayawapi wakuu wa shule nafasi ya kuweka maono.** Mara nyingi wakuu wa shule huwekewa matarajio makubwa mno. Wakuu wa shule ni muhimu sana katika utekelezaji bora wa mabadiliko. Katika baadhi ya nchi, wanachunguzwa sana pia kutokana na mbinu mpya za kufuatilia uwajibikaji. Hata hivyo, utafiti uliofanyiwa wakuu wa shule katika nchi 14 zenye mapato ya wastani ulionyesha kwamba wanatumia asilimia 68 ya wakati wao kufanya taratibu za kawaida za usimamizi. Kama theluthi moja ya wakuu wa shule za umma na humusi ya wakuu wa shule za kibinafsi katika nchi za OECD waliripoti kukosa muda wa kutosha wa kutoa uongozi elekezi.

### Viongozi wa shule hawafai kuwa mashujaa. Kushirikiana uongozi hukuza shule bora.

- **Kushirikiana uongozi kote shuleni hukuza mazingira ya kujifunza yenye ushirikiano.** Hali hii huwawezesha walimu kuongoza katika madarasa yao, wanafunzi kuwa viongozi wanaohudumu kati ya wenzao, na wazazi na wanajamii kuhusika. Hata hivyo, kati ya vipengele vinne vya uongozi, ushirikiano ndicho kipengele ambacho hakisisitizwi sana katika mipango ya mafunzo.
- **Uongozi wa shule mara nyingi ni wa ngazi.** Manaibu wakuu wa shule na walimu wanaweza kusaidia kutimiza malengo ya shule wanapowezeshwa kwa kupewa wajibu bayana, mafunzo na vichocheo. Lakini ni nusu tu ya nchi zinasisitiza bayana ushirikiano na walimu katika viwango vyao vya uongozi na ni kama theluthi ya mipango ya mafunzo ya uongozi inazingatia suala hili. Kama asilimia 81 ya nchi zimeifanya sharti kwa bodi za shule kujumuisha walimu, asilimia 83 kujumuisha wazazi, asilimia 62 kujumuisha wanajamii na asilimia 57 kujumuisha wanafunzi.

### Viongozi wa mifumo hawazingatiwi vya kutosha katika mipango ya uongozi.

- **Maafisa wa elimu katika ngazi za kati na za mashinani wanaweza kuwa viongozi.** Wanaweza kuleta mabadiliko ya kuboresha sekta nzima na upatano katika marekebisho ya elimu na sera. Nchi zinazidi kutambua kwamba maafisa hawa wanaweza kuwa na ushawishi zaidi wakipewa uhuru zaidi wa kufanya maamuzi.
- **Viongozi wa mifumo huwa na ufanisi wanapofanya kazi na wahusika wengine.** Katika jimbo la Mexico la Puebla, mafanikio katika mageuzi ya elimu yalitokana na juhudi za pamoja katika mfumo mzima ambazo zilijumuisha uongozi wa maafisa wa elimu.

### Mawaziri wa elimu hufanya kazi katika mazingira changamano ya kisiasa na hukumbwa na kizuizi cha hatamu fupi.

- **Mawaziri huweka uwiano kati ya matakwa mengi katika hatamu fupi na mara nyingi hawana tajiriba ya ualimu.** Hifadhidata mpya ya kimataifa inaonyesha kwamba nusu ya mawaziri wa elimu wa tangu mwaka wa 2010 huondoka kwenye wadhifa huo ndani ya miaka miwili baada ya kuteuliwa, vilevile, ni asilimia 23 pekee wana tajiriba ya kufunza katika shule.
- **Viongozi wa kisiasa wanahitaji kuwa na busara ya kuleta mwafaka wa kisiasa na kujenga mahusiano ili kuleta mageuzi.** Kujenga miungano na mahusiano kunaweza kuziba pengo la ukosefu wa muda wa kutosha na data bora na kunapokuwa na maoni kinzani.
- **Hatamu fupi huifanya vigumu kutekeleza mageuzi.** Uchambuzi wa miradi ya elimu ya Benki ya Dunia kati ya mwaka wa 2000 na 2017 katika nchi 114 ulipata uhusiano hasi wa maana katika ya kubadilishwa kwa mawaziri na matokeo ya miradi.

### Kuwa na wanawake zaidi katika uongozi kunaweza kuleta matokeo mema katika elimu.

- **Viongozi wa kisiasa wanawake wamewekea elimu kipaumbele kuliko wenzao wanaume.** Wabunge wanawake wamesaidia kuongeza fedha zinazotolewa kwa elimu ya msingi duniani kote. Hata hivyo, asilimia ya mawaziri wanawake iliongezeka kutoka asilimia 23 katika kipindi cha 2010-2013 hadi asilimia 30 tu katika kipindi cha 2020-2023.
- **Baadhi ya tafiti zinaonyesha kwamba wanawake hupata matokeo bora ya mafunzo kama wakuu wa shule kuliko wanaume.** Katika nchi za Afrika zinazotumia kifaransa, wanafunzi katika shule za msingi zinazoongozwa na wakuu wa shule wanawake waliwashinda walio katika shule zinazoongozwa na wakuu wa shule wanaume katika hisabati na kusoma kwa angalau miezi sita.
- **Ijapokuwa wanawake wengi hufunza, wachache zaidi huongoza shule.** Kwa wastani, sehemu ya wakuu wa shule wanawake katika elimu ya msingi na sekondari iko chini kwa angalau pointi 20 za asilimia ikilinganishwa na sehemu ya wastani ya walimu wanawake. Ni asilimia 11 tu ya nchi duniani zimeweka mikakati ya kushughulikia suala la uwakilishi wa jinsia katika uteuzi wa wakuu wa shule.

### Wahusika wengi huongoza kwa kushawishi mwelekeo wa mifumo ya elimu.

- **Vyama vya walimu, vyama vya wanafunzi, viongozi wa biashara, wasomi na asasi za raia huwajibisha serikali, hufanya utetezi na ufahamishaji.** Ushawishi ni muhimu: Nchini Marekani, baadhi ya majopo ya washauri hayana uzito sana kwa upande wa ujuzi lakini yana uzito mwingi katika majadiliano ya elimu katika Bunge; hali ni kinyume cha hiyo kwa mengine.
- **Mashirika ya kimataifa husaidia kuelekeza na kutoa ushauri katika mjadala wa kimataifa kuhusu elimu, pamoja na kufadhili mifumo ya elimu ya nchi mbalimbali.** Hata hivyo, kushindania nafasi na ushawishi kunaweza kuyavuta mbali na lengo la kuboresha elimu na mamlaka yao yanaweza kudhoofishwa na ukosefu wa ujuzi au wa ufanisi.

**Viongozi wa elimu wa elimu mara nyingi hawachukuliwi kuwa wa maana vile.** Ilhali, wanaelekeza shule, vyuo vikuu, idara na wizara zao, kwa njia ambazo mara nyingi hazionekani. Mitindo yao ya uongozi hudhihirisha hulka na ujuzi wao, lakini pia hubadilika kulingana na sifa za timu zao, malengo ya asasi zao na muktadha ambamo wanafanyia kazi. Utofauti wa mitindo ya uongozi ndiyo sababu hasa ya kutokuwepo kwa njia rahisi ya kuonyesha jinsi wanavyoathiri elimu. Ndiyo sababu pia athari hizo mara nyingi hupuuzwa. Hata hivyo, kuna hitaji kubwa la viongozi bora wa shule, mifumo na siasa kwa sababu changamoto za elimu zingali kubwa.

**Uongozi mara nyingi huhusishwa na siasa na biashara.** Vitabu maarufu kuhusu usimamizi hutoa mifano mingi ya kuzingatia ujuzi, hulka, tabia, mitindo, motisha na maadili ya viongozi, mara nyingi vikiwaonyesha kama watu wa kipekee. Katika mfano mmoja kama huo, orodha ya vipengee tano inaeleza 'wanachofanya viongozi wenye ufanisi'. Mwandishi anasema kwamba wao huweka viwango vya ubora na ni mfano kwa wengine ('huonyesha njia'); huweka maono ya hali bora zaidi ambayo shirika linaweza kufikia ('hukuza maono ya pamoja'); hutafuta njia zenye ubunifu za kuboresha shirika ('huhoji michakato'); hukuza ushirikiano, hujitahidi kukuza mazingira ya kuaminiana na kumfanya kila mtu ajihisi kwamba anaweza ('huwawezesha wengine kutenda') na hutambua michango ya watu binafsi ('huhimiza moyo').

**Uongozi umefafanuliwa kama 'mchakato wa ushawishi wa kijamii, ambao hutumia juhudi za wengine kikamilifu kwa madhumuni ya kutimiza lengo'.** Ufafanuzi huu unadokeza mambo mawili: kwanza, uongozi hautunukiwi moja kwa moja kwa kuwa na cheo cha mamlaka bali ni kwa kuwa na uwezo wa kuathiri vitendo vya watu wengine, na pili, uongozi huangaliwa katika muktadha wa lengo. Viongozi hutekeleza wajibu muhimu katika kubainisha lengo hilo ambalo wanatimu, shirika au jamii inaweza kuungana kulitimiza. Katika uwanja wa elimu, ufafanuzi wa hivi majuzi unalandana na dhana hizi mbili: 'uongozi ni utetezi wa mbinu mahususi ya uratibu': 'utetezi' unawakilisha mchakato wa ushawishi, huku 'mbinu ya uratibu' unadokezea lengo. Kwa sababu uongozi katika elimu unahusisha malengo mahususi, mchakato wa ushawishi wa kuwahamasisha watu kutimiza malengo hayo, fursa lakini pia vikwazo vya kuyatimiza, maswali matatu yanaibuka:

**Viongozi wa elimu hujitahidi kutimiza malengo yapi?** Ripoti hii inatoa wito kwa wote wenye shauku ya elimu: #OngozaKatikaElimu. Kubainisha malengo ya mafunzo ni mchakato wa kisiasa unaowahusisha wadau wote wa elimu. Kuna dhana fulani – ambayo hata ripoti hii inachangia bila kukusudia, ukizingatia wajibu wake wa kuripoti kuhusu viashiria vya elimu vinavyoweza kulinganishwa – kwamba malengo ya mafunzo yanaweza kuwekewa mipaka ya mkusanyiko wa matokeo yanayoweza kupimwa katika masomo kama vile kusoma, hisabati na sayansi. Hata hivyo, elimu ina malengo mapana zaidi ya mafunzo: si uwasilishaji wa maarifa na upataji wa ujuzi unaoleta kufuzu tu, bali pia ni kuwawezesha wanafunzi kuwaza na kutenda kwa kuwajibika na kuwafundisha mila na desturi za pamoja. Hatua ya kwanza katika mjadala wowote wa uongozi katika elimu inastahili kuwa kubainisha kusudi.

**Viongozi wa elimu hujitahidi vipi kutimiza malengo haya?** Ukuaji wa shule na taasisi nyingine za elimu kuwa mashirika makubwa na kubadilika kwa michakato rahisi ya elimu kuwa mifumo changamano katika nchi zilizostawi kumezua shauku katika uwanja wa utawala na usimamizi wa elimu. Hata hivyo, nafasi ya viongozi wa elimu ilijumuishwa katika uchambuzi huo, huku watafiti wakichambua mafanikio ya viongozi kama kazi ya mabingwa. Hatua kwa hatua, mbinu zenye taratibu za kisayansi zilianza kutumika, zikianza kuwazia uongozi kama kipengele cha usimamizi wa elimu ambacho yamkini kinabainika. Watafiti waliamini kwamba wanaweza kutambua vitendo vya watu binafsi na mipangilio ya shirika inayohusiana na uongozi, hali iliyoibua hoja kwamba vigezo hivi viwili haviwezi kuwaziwa kila kimoja kivyake kwa sababu watu binafsi ndio huunda shirika. Hivi karibuni, utekelezaji wa uongozi umetambuliwa kuwa unaelekezwa na **mahusiano** ya kijamii katika taasisi na mifumo hii ya elimu. Wanaofanya kazi katika sekta ya elimu hutegemeana, kwa hivyo majukumu ya uongozi yanahitaji kugawanywa ili kutimiza malengo ya elimu.

**Viongozi wa elimu wanaweza kukabiliwa na vikwazo vipi?** Walio na nyadhifa za uongozi katika elimu wanahitaji kuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu wanayotarajiwa kuyatekeleza. Lakini **muktadha** ni muhimu pia. Kanuni na kaida rasmi na zisizo rasmi za kijamii, kiuchumi, kisiasa na za utamaduni hupanua au kuzuia ari ya kujituma ya viongozi wa elimu na upeo wa mambo wanayoweza kufanya. Uhuru wao wa kufanya maamuzi unatokana na kanuni za utawala na uwajibikaji, ambazo ni tofauti sana katika nchi mbalimbali, mara nyingi zikidhihirisha kaida za kitamaduni. Fursa za kuongoza pia zinatofautiana baina ya nchi, hasa miongoni mwa taasisi za elimu. Kila shule ya chekechea, shule, taasisi ya mafunzo ya kiufundi, chuo, chuo kikuu na kituo cha mafunzo ya watu wazima kipo katika muktadha tofauti na viongozi wake huwekewa matarajio tofauti na jamii wanayoihudumia. Taasisi za elimu, ndogo au kubwa, za umma au za kibinafsi, za mijini au za mashambani, zenye rasilimali nyingi au haba, zote hukabiliana na hali tofauti. Taasisi zinazofanya kazi katika miktadha ya dharura au katika jamii zenye makabila au lugha mbalimbali zinahitaji viongozi wawe na ufahamu wa kina na waelekevu kwa mazingira yao.

**Viongozi wa elimu wanaweza kutatanishwa na matokeo mbalimbali.** Inawezekana kwamba kuzingatia kuboresha matokeo ya mafunzo yanayoweza kupimwa, ambayo ndiyo matokeo hutathminiwa na tafiti nyingi, kunaweza kuathiri vibaya maboresho katika matokeo mengine mengi ya elimu, kama vile kukuza mazingira jumuifu au kutayarisha wanafunzi kuendana na changamoto za siku zijazo za uraia na mabadiliko ya tabianchi. Tathmini za utendakazi zilizosawazishwa zina hatari ya kuleta mbinu sawa za usimamizi na uongozi, hali ambayo huenda isifae miktadha mahususi. Ijapokuwa ripoti hii inaangalia jinsi nchi zimeshughulikia suala la viwango vya uongozi, inalenga tu kuelezea juhudi zao wala si kuelekeza maudhui au utekelezaji wake.

**Je, ni watu binafsi au timu bora huleta matokeo katika elimu?** Wanaokosoa wanasema kwamba watu binafsi wamepewa uzito kupita kiasi – na wanadokeza kwamba uongozi umeibuka kutoka wajibu usiojitanguliza hadi kutajwa kama kigezo cha pili muhimu zaidi kinachoeleza matokeo ya mafunzo. Huenda ni wazo la kupotosha kudhani kwamba ni juhudi za watu binafsi pekee ambazo hubadilisha mifumo ya elimu – mwelekeo ambao huenda umejikita katika utamaduni wa Magharibi. Mazingira yanayofaa ya taasisi na miundo bora ya mashirika huenda vikawa vigezo muhimu zaidi. Hii haimaanishi kwamba wakuu wa shule hawatekelezi jukumu muhimu sana, bali kwamba jukumu hili lina vipengele vingi. Kuchunguza utendakazi wa taasisi ya elimu kwa kina kunaweza kuonyesha kwamba tokeo njema la elimu huenda lilitokana na kazi ya watu kadhaa wenye kujituma ambao walijitolea na kuchangia ujuzi wao. Kuwaonyesha watu hawa kama wafuasi wanaomtegemea kiongozi ni kudunisha michango yao.

**Kuna tofauti kati ya kudhibiti watu na kuwawezesha kufanya maamuzi.** Ukinzani mwingine ni kati ya masharti na uwezo wa kutenda kulingana na hali bila kujali masharti yoyote. Ijapokuwa uwezo wa viongozi na sifa zao binafsi ni muhimu, yote haya yanaweza tu kutumika vyema katika mazingira yanayofaa. Viongozi pia hufanya kazi katika miktadha yenye vikwazo. Ijapokuwa baadhi ya viongozi wana rasilimali za kutekeleza mipango yao, inawabidi wengine kutafuta suluhisho katika hali ngumu. Uhuru unaweza kuwaruhusu viongozi wa elimu kutenda, lakini haimaanishi kwamba wanatenda kwa ajili ya masilahi yao wenyewe badala ya kuelekea lengo la pamoja la kuleta matokeo bora.

**Ijapokuwa uongozi ni dhana ya kuvutia, ripoti hii inatambua kwamba si dhana bayana kabisa.** IMara nyingi huwa vigumu kutofautisha kiongozi bora na msimamizi bora. Licha ya malengo makuu, kazi ya viongozi wa elimu mara nyingi huwa ya kutosisimua. Wakuu wa shule wanahitaji kusimamia bajeti za shule au kufanya mikutano ya kufanya maamuzi ya adhabu. Wakuu wa idara na walimu viongozi yamkini hutumia muda mwingi wakitayarisha ratiba na kupanga michakato ya kuajiri walimu. Maafisa wa elimu nyanjani watasumbuka kuhakikisha vitabu vya kiada vimefika kwa wakati au kulipa marupurupu ya kujikimu kwa walimu wanaosafiri kwenda kupata mafunzo. Mawaziri watahitaji kuwajibu wakazi wa maeneo yao ili kutimiza maombi madogo au kujikinga dhidi ya kukosolewa na vyombo vya habari kuhusiana na kosa la ofisa fulani. Majukumu yote haya ya kawaida mara nyingi hayahusishwi na viongozi. Hata hivyo, kuratibu shughuli za kila siku kwa ufanisi ili kutenga wakati wa kupanga kwa ajili ya siku za usoni ni jukumu muhimu sana la viongozi. Katika hali halisi, kuna mfuatano wa shughuli na tofauti kati ya usimamizi na uongozi wa elimu inaweza kuwa ya kulazimisha.

**Je, ni lazima uongozi uhusishwe na mabadiliko?** Baadhi wanatoa hoja kwamba uongozi unahusu kuwa kichocheo cha mabadiliko, na kwamba usimamizi unahusu kudumisha hali jinsi ilivyo huku uongozi ukiwa unahusu kuibadilisha. Usimamizi wa mabadiliko hurejelea kutekeleza mabadiliko ambayo yameafikiwa. Uongozi wa mabadiliko unahusu haja ya mabadiliko na kuwahamasisha watu kuunga mkono mabadiliko hayo. Licha ya hayo, ni muhimu kuuliza ikiwa mabadiliko yote huwa mema au kama kupinga mabadiliko, hasa yanayolazimishwa kutoka nje, pia ni ishara ya uongozi. Mchambuzi mmoja ameeleza, 'Sifa moja ya nyakati ya hivi majuzi imekuwa mabadiliko ya mara kwa mara yanayoelekezwa kwenye shule: msururu wa harakati mapya, mipango mipya na mielekeo mipya. Inasikitisha kwamba baadhi katika ngazi zote za elimu wanaonekana daima kukimbilia lolote jipya linalokuja … Hata hivyo, si sahihi kabisa kuchukulia kwamba shule ina ufanisi iwapo inabadilika tu … Tunahitaji kukumbushwa kwamba mabadiliko kwa ajili ya kuwa na mabadiliko tu, ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya teknolojia, si sharti yawe mema; ni sharti yaongozwe na hekima, ukarimu na haki'.

**Je, ni lazima uongozi uhusishwe na ushawishi?** Kwa ujumla, uongozi hudhaniwa kwa njia chanya. Hata hivyo, vyanzo vyake (ambavyo vinaweza kujumuisha nguvu) na mbinu zake (ambazo zinaweza kujumuisha hila) zinaweza kudhaniwa kwa njia hasi. Vivyo hivyo, hata 'ushawishi' unaweza kuonekana kama dhani chanya au hasi. Mchambuzi mmoja aliuliza: 'ikiwa uongozi ni aina, au kipengele cha ushawishi, je hilo halimaanishi kwamba 'uongozi' hauhitajiki?' Yaani, kama kwa kweli tunazungumzia ushawishi, mbona tusijikite katika neno hilo tu? … Kwa ufupi, wakati wa kueleza na kuchambua mtiririko wa vitendo vya pamoja na vitendo vya watu kama sehemu ya mchakato huo, mbona tunazungumzia uongozi wala si ushawishi au nguvu?'

## JEDWALI LA 1:
### Vipengele vinne vya uongozi wa shule vinaeleza desturi muhimu za wakuu wa shule

| Vipengele | Vigezo vinavyoashiria |
|---|---|
| Bainisha matarajio | Buni, wasilisha na ufafanue maono, azma na malengo ya pamoja, ikiwa ni pamoja na kuzingatia mafanikio ya wanafunzi<br>Weka matarajio ya juu kwa wafanyakazi na wanafunzi<br>Toa motisha ya kutia moyo, huku ukishawishi kwa kuweka mfano binafsi na kuwakilisha jamii<br>Fahamu yanayojiri na utumie data kufanya maamuzi |
| Zingatia ufunzaji | Zingatia maendeleo ya ufunzaji, k.m. kupitia usimamizi wa walimu<br>Toa rasilimali na nyenzo za ufunzaji na uzisawazishe na malengo ya ufunzaji<br>Panga, ratibu na utathmini mtalaa<br>Linda wafanyakazi dhidi ya mambo yanayowavuta fikra kazini<br>Fuatilia maendeleo ya wanafunzi |
| Kuza ushirikiano | Kuza utamaduni wa shule na mazingira chanya<br>Dumisha mazingira salama na yenye afya shuleni<br>Kusanya rasilimali kimkakati, kuza mahusiano na udhibiti hatari<br>Endeleza ushirikiano, hasa baina ya walimu, na uwawezesha kuchukua hatua<br>Jenga uhusiano na ushauriane na familia na jamii |
| Endeleza watu | Fuatilia mahitaji ya walimu ya maendeleo ya kitaaluma<br>Wape walimu usaidizi binafsi wa kitaaluma na nafasi za kupata ulezi<br>Tathmini walimu na utuze kazi nzuri<br>Changamsha fikra<br>Jenga mahusiano ya kuaminiana na udhibiti mizozo<br>Kuwa unapatikana |

*Chanzo: Leithwood (2012) na Leithwood na wengine (2020a).*

**Uongozi unajitokeza zaidi kati ya sababu za mafanikio katika elimu:** Hoja ni pamoja na: ‘Kati ya vigezo vyote vinavyochangia wanafunzi wanchojifunza shuleni … uongozi upo katika nafasi ya pili baada ya mafunzo ya darasani tu. Isitoshe, uongozi bora una athari kubwa zaidi katika hali ambapo unahitajika zaidi (k.m. katika shule ‘zilizo taabani’). Ushahidi huu unaunga mkono shauku iliyotanda nyakati hizi ya kuboresha uongozi kama kigezo muhimu katika utekelezaji wa mageuzi’, na ‘Kwa kweli hakuna matukio yaliyorekodiwa ya shule zilizo taabani kubadilishwa bila kiongozi shupavu kuingilia kati’. Ripoti hii inanuia kuchambua jinsi maarifa haya yanaweza kutumika kuwasaidia wanaofanya maamuzi kuunda sera zitakazohakikisha kwamba kila taasisi na ofisi ya elimu itakuwa na viongozi ambao wametayarishwa kushughulikia na kutatua matatizo ya elimu kwa ustadi. Hili linaondoa mwanga kwenye watu wa kipekee na kuuweka kwenye michakato ya kimfumo.

**Dhana ya uongozi wa shule na mitazamo kuhusu wajibu wa viongozi imekuwa ikibadilika.** Kwa jumla, mtazamo umebadilika kutoka kumwona mkuu wa shule kama anayetekeleza majukumu ya usimamizi na urasimu hadi kutarajia ahusike zaidi katika kufanya kazi na walimu na wafanyakazi wengine ili kuboresha ‘matokeo’ ya shule. Matarajio kuhusu aina ya matokeo haya yanaelekezwa na mapendeleo ya kijamii na dhana za mamlaka za elimu na jumuiya ya elimu, ikiwa ni pamoja na viongozi wenyewe. Vipengele vitatu vya uongozi wa shule – kubainisha matarajio, kuzingatia ufunzaji na kukuza ushirikiano – vinalingana kwa ujumla na dhana tatu za uongozi – uongozi wa kimageuzi, elekezi na uliosambazwa – ambazo zimezingatiwa katika utafiti, na kipengele cha nne ambacho kinahusiana kwa karibu na dhana zote tatu:

- Kubainisha matarajio kunahusiana na uongozi wa kimageuzi, unaojumuisha tabia zinazowashawishi,

kuwahimiza na kuwahamasisha washiriki wa jumuiya ya shule kuboresha shule hiyo.

- Kuzingatia ufunzaji kunahusiana na uongozi elekezi, unaojumuisha tabia zinazowashawishi, kuwahimiza na kuwahamasisha washiriki wa jumuiya ya shule kuboresha matokeo ya mafunzo.
- Kukuza ushirikiano kunahusiana na uongozi uliosambazwa au wa pamoja, ambao unarejelea jinsi viongozi huingiliana na kushirikiana na watu wengine na kushiriki wajukumu yao.
- Kuendeleza watu ni sehemu ya majukumu ya usimamizi wa rasilimali watu ya viongozi wa shule, lakini linawahitaji pia wasaidie timu zao kujifunza na kukua.

Katika kila kimoja kati ya vipengele hivyo vinne, viongozi bora wameonekana kutumia mkusanyiko wa desturi za msingi **(Jedwali la 1)**. Kwa kweli, tofauti katika desturi hizi ni muhimu kwa wakuu wa shule na viongozi walimu, lakini pia kwa viongozi wa mifumo, hasa katika ngazi ya mtaani. Vipengele hivi vinne vya uongozi vimezingatiwa kote katika ripoti hii.

## UONGOZI WA SHULE: WAJIBU, ATHARI NA VIWANGO

**Katika nyakati zilizopita, wakuu wa shule sanasana wamechukuliwa kama wasimamizi, lakini zaidi na zaidi wanatarajiwa kutekeleza wajibu wenye athari pana zaidi.** Wakuu wa shule wanahitaji kuwa na umahiri mbalimbali ili kutekeleza majukumu haya. Wanahitaji uwezo wa kutumia data, kuweka vipaumbele, kupanga, kutekeleza, kusimamia na kutathmini ili kusuluhisha matatizo. Wanahitaji kuwasiliana kwa ufanisi ili kukuza uelewa wa pamoja, kuhamasisha timu kuhusiana na malengo na kukuza maendeleo ya kitaaluma. Wanahitaji kuwa na werevu wa kihisia, kujitambua, ufahamu wa kijamii na ujuzi wa kujidhibiti ili kukuza mahusiano ya maana.

**Wakuu wa shule wanatarajiwa kuweka maono kwa ajili ya jumuiya ya shule.** Duniani, asilimia 78 ya nchi zimetaja ujuzi huu katika viwango vyao vya kitaifa. Nchi za Brunei Darussalam na Malesia zinasisitiza haja ya wakuu wa shule kuwa na ujuzi wa maono na upangaji mikakati ili kuchangia ubora wa taasisi. Wakuu wa shule pia wanatarajiwa kudumisha viwango vya maadili katika kutekeleza uongozi wao na inapowezekana, kutoa motisha na kuongoza kwa kuwa mfano. Kazakhstan inasisitiza kwamba wakuu wa shule wanastahili kutohimili ufisadi na udanganyifu wa kimasomo.


**Wakuu wa shule hutarajiwa kuwa viongozi wa kuelekeza. Duniani kote, asilimia 57 ya nchi zinatarajia wakuu wa shule watoe maoni kwa walimu kulinganana na jinsi wanavyoona hali.** Lakini vitendo katika hali halisi vinaweza kuwa tofauti na matakwa ya kanuni zilivyoandikwa. Uchunguzi wa nchi 14 zenye mapato ya chini na ya wastani, zikiwemo Ecuador, Pakistan na Ufilipino, ulionyesha kwamba wakuu wa shule walitumia asilimia 68 ya muda wao katika shughuli za usimamizi. Ushahidi kutoka Mpango wa Kutathmini Wanafunzi wa Kimataifa (PISA) unadokeza kwamba uangalizi wa shughuli za ufunzaji umepungua kidogo katika miaka ya hivi majuzi. Asilimia ya wakuu wa shule za sekondari katika nchi za OECD walioripoti kwamba wao wenyewe au wafanyakazi wakuu waliangalia masomo ilipungua kutoka asilimia 81 katika mwaka 2015 hadi asilimia 77 katika mwaka wa 2022 **(Mchoro wa 1).**

**Wakuu wa shule wanatarajiwa kukuza ushirikiano.** Nusu ya nchi zinawataka wakuu wa shule wakuze ushirikiano wa walimu, kwa mfano, kwa kuendeleza ushirikiano wa ndani kupitia jumuiya za mafunzo ya kitaaluma, kupanga kwa ushirikiano, miradi ya wanataaluma mbalimbali, timu za walimu na maoni ya wenzi. Nchini Vietnam, wakuu wa

**MCHORO WA 1:**

**Wakuu wa shule wameripoti kupungua kwa muda wanaotumia katika uangalizi wa shughuli za ufunzaji katika nchi zenye mapato ya juu**

*Asilimia ya wakuu wa shule za sekondari wanaoripoti kufanya shughuli zilizobainishwa za uangalizi wa ufunzaji, nchi za OECD, 2015 na 2022*




*GEM StatLink:* https://bit.ly/GEM2024_Summary_fig1
*Chanzo:* OECD (2023).

shule huanzisha timu za kitaaluma za walimu wakiwa katika vikundi kulingana na darasa au somo wanalofunza ili kuzingatia masuala kama vile teknolojia, kuwasaidia wanafunzi wenye ulemavu, ushauri shuleni, kubuniwa kwa mipango ya elimu shuleni na uchaguzi wa vitabu vya kiada.

**Wakuu wa shule wanatarajiwa kusaidia wafanyakazi kukua.** Duniani, asilimia 70 ya nchi ziliwakabidhi wakuu wa shule jukumua la kutathmini walimu kwa ajili ya malengo kama vile kupandishwa cheo, maendeleo ya kikazi, uhakikisho wa ubora na uwajibikaji. Katika mifumo 48 ya elimu iliyoshiriki katika Utafiti wa Kimataifa wa Ufundishaji na Kujifunza (TALIS) wa 2018, asilimia 71 ya walimu walitathminiwa rasmi na wakuu wa shule zao kila mwaka. Mbinu za tathmini zilikuwa ni pamoja na kuchambua matokeo ya wanafunzi (94%), kuwatafiti wanafunzi (82%), kuthamini ujuzi wa maudhui wa walimu (70%) na tathmini za kujifanyia (68%). Uchambuzi wa nchi 45 kwa kutumia data kutoka kwenye Utafiti wa Kimatifa wa Mienendo katika Hisabati na Sayansi (TIMSS) wa mwaka wa 2015 ulipata kwamba walimu waliridhika zaidi na kazi yao wakati viongozi wa shule walikuwa wanapatikana na kuunga mkono upangaji wa taasisi.

**Wakuu wa shule wanaweza kuathiri pakubwa matokeo mbalimbali ya wanafunzi na walimu.** Ni vigumu sana kutathmini athari ya wakuu wa shule. Upande wa mchango, ni vigumu kutazma na kupima vitendo. Vitendo pia huingiliana vyenyewe na pia huingiliana na muktadha. Upande wa matokeo, kuna vigezo vingi vya kufuatilia – wanafunzi, walimu, shule na jamii. Matokeo pia ni mengi. Hata hivyo, tafiti nyingi zinalimbikiza ushahidi wa athari ya desturi mahususi za uongozi kwenye miundo, utamaduni na walimu wa shule.

**Tafiti nyingi zinazingatia athari ya wakuu wa shule kwenye kujifunza kwa wanafunzi, ambayo ni rahisi zaidi kupima.** Uchambuzi wa shule 1,800 katika nchi nane ulipata kwamba kuboresha kigezo fulani cha ubora wa usimamizi kwa alama moja ya mkengeuko wastani kuliimarisha matokeo ya wanafunzi kwa alama 0.23 hadi 0.43 za mkengeuko wastani. Utafiti uliofuatilia zaidi ya walimu wakuu 20,000 huko Uingereza kutoka mwaka wa 2004 hadi 2019 ulionyesha kwamba kumwondoa mwalimu mkuu dhaifu (kutoka asilimia 16 ya chini) na badala yake kumweka mwalimu mkuu hodari (kutoka asilimia 15 ya juu) kuliimarisha matokeo kwa alama mbili katika masomo yote au kwa alama moja katika somo moja katika shule za sekondari. Huko Haiti, wakuu wa shule kuboresha desturi za kawaida za usimamizi kuliimarisha pakubwa alama za kusoma katika madarasa ya awali kwa alama 0.43 za mkengeuko wastani katika shule zilizoharibiwa vibaya na Kimbunga Matthew.

**Tafiti pia zinaonyesha athari ya wakuu wa shule kwenye matokeo mengine mbalimbali ya elimu.** Wakuu wa shule wanaweza kuathiri sana kuhudhuria na kubaki shule kwa wanafunzi. Katika jimbo la Victoria nchini Australia, juhudi za pamoja za wakuu wa shule ziliongeza viwango vya kuhudhuria shule kutoka asilimia 86.5 katika mwaka wa 2022 hadi asilimia 88.6 katika mwaka wa 2023, jambo liliopunguza pengo la uhudhuriaji kati ya shule za aina tofauti. Wakuu hodari wa shule hukuza mazingira ya kutia moyo yanayoendeleza ustawi wa kihisia wa wanafunzi. Nchini Jamaika, wakuu wa shule za sekondari wana jukumu katika kuajiri washauri zaidi, kutenga fedha za kuwasaidia wanafunzi na wafanyakazi na kuhakikisha kwamba nyenzo kama vile miradi ya kutoa kifungua kinywa zinapatikana. Wakuu wa shule pia hufuata desturi zinazozingatia utamaduni ili kukuza mazingira jumuifu, kama vile huko Malta, ambapo wameendeleza utamaduni jumuifu wa shule ili kusaidia familia na wanafunzi wahamiaji.

**Sifa binafsi, za shule na mfumo huathiri uongozi wa wakuu wa shule na mchango wao katika mafanikio ya wanafunzi.** Nchini Afrika Kusini, wakuu wa shule wanawake wametambuliwa kwa kujenga mazingira ya elimu ambayo ni salama na ya ushirikiano zaidi, pamoja na majukumu bayana zaidi ya wafanyakazi. Wakuu wa shule katika shule zilizo katika hali ngumu nchini Argentina walikuwa na chini ya nusu ya miaka ya tajiriba ikilinganishwa na wenzao katika shule zisizo katika hali ngumu. Miongoni mwa nchi 20 zilizoshiriki katika utafiti wa PISA wa mwaka wa 2022, kadri wakuu wa shule wanavyokuwa na wajibu wa msingi juu ya maamuzi ya rasilimali watu na za kifedha, ndivyo uwezekano unavyoongezeka kwamba nchi husika itakuwa miongoni mwa zile zilizowekwa kwenye daraja la juu zaidi kulingana na matokeo ya wastani katika hisabati. Hata hivyo, majukumu mengi mno bila rasilimali za kutosha yanaweza kuleta mfadhaiko na changamoto.

**Viwango vya uongozi vinaweza kuelekeza vitendo na uthibitishaji.** Duniani, asilimia95 ya nchi zimeidhinisha viwango, ama kupitia sheria na sera au katika hati za kujisimamia. Nchini Rwanda, Viwango vya Kitaaluma vya Uongozi Bora wa Shule vya 2020 vinabainisha wajibu na ujuzi muhimu, ikiwa ni pamoja na uelekezaji wa kimkakati, kuongoza ujifunzaji na ufunzaji, kusimamia shule na kushirikiana na jamii. Ni nusu tu ya nchi zina viwango kwa ajili ya wakuu wa shule vinavyotaja bayana kuunga mkono ushirikiano na walimu. Lakini viwango vya uongozi vimekosolewa kwa kupuuza tofauti katika miktadha na kwa kutegemea sana mifumo ya Magharibi.

## UONGOZI WA SHULE: UTEUZI, MATAYARISHO NA MAZINGIRA

**Utaalamishaji wa kazi ya wakuu wa shule ni muhimu sana ukizingatia ugumu wa majakumu ya kazi hiyo.** Ili kazi hii ikue kufikia hadhi ya taaluma, kuna haja ya kanuni za ajira na uteuzi ambazo ni bayana, wazi na zinazotegemea ustahilifu, mafunzo yanayofaa na fursa za maendeleo, ikiwa ni pamoja na usaidizi katika hatua za mwanzo na mazingira mazuri ya kazi ili kuimarisha kiwango cha kuridhika kazini na fahari ya kazi hii.

**Kuna haja ya kuboresha michakato ya uteuzi ili kutaalamisha kazi ya wakuu wa shule.** Bila kuzingatia kiwango cha uhuru kilichopewa shule, vigezo visivyo na upendeleo, vya haki, jumuifu, wazi na bayana vinaimarisha kuaminika kwa nafasi ya mkuu wa shule na kuboresha matokeo. Kuwapandisha cheo wafanyakazi wa ndani husisitiza ufahamu na uelewa wa utamaduni, michakato na changamoto za shule. Michakato wazi ya ajira inaweza kuvutia watafutakazi wa nje wenye ujuzi na mitazamo mipya kuhusu ukuaji wa shule.

**Michakato ya kuteua wakuu wa shule inaanza kuwa yenye ushindani.** Michakato ya ajira ya ndani na ya wazi inaweza kutumia ushindani kutathmini watafutakazi. Duniani, asilimia 63 ya nchi hutumia michakato wazi ya ajira ambayo ina ushindani katika elimu ya msingi na ya sekondari, huku asilimia nane zikitumia michakato wazi ya ajira ambayo ina ushindani katika elimu ya msingi pekee na asilimia tatu katika elimu ya sekondari pekee. Nchini Romania, mchakato wenye ushindani wa kuteua wakuu wa shule umeimarisha matokeo ya wanafunzi. Katika Jamhuri ya Korea, aina tatu za michakato ya ajira zimetumika kwa pamoja. Katika mwaka wa 2012, asilimia 68 ya uteuzi ulifanyika 'kupitia mwaliko' kwa shule za kawaida, asilimia 30 ulikuwa 'wa ndani' (kupandishwa cheo) katika shule za kujitegemea, na asilimia 2 ulikuwa wazi, kiwango ambacho kiliongezeka hadi asilimia 10 kufikia mwaka wa 2022.

**Michakato ya kuajiri na kuteua wakuu wa shule inaweza kuwa ya kisiasa.** Wanasiasa kuwa na mamlaka ya kuteua wafanyakazi ni jambo la kawaida katika sekta ya umma katika nchi nyingi. Nchini Brazil, ambapo mbinu mbalimbali za kuteua wakuu wa shule zinaweza kuwepo katika kila jimbo, njia za uteuzi zilizotumika sana kwa mpangilio wa kushuka zilikuwa upigaji kura (asilimia 56), uteuzi wa kisiasa (asilimia 48) na uteuzi kufuatia kuwasilisha hati ya pendekezo ('mpango wa usimamizi') (asilimia 33) au kwa kutegemea kuhitimu na vyeti (asilimia 30). Huko Georgia, uwezekano wa kuwepo kw ushawishi wa wanasiasa katika uteuzi wa wakuu wa shule umekuwa suala muhimu katika maandamano ya wanafunzi.

**Vigezo vya kuteua wakuuu wa shule vinazidi kuwa vikali zaidi.** Duniani, asilimia 46 ya mifumo ya elimu inahitaji wanaotaka kuwa wakuu wa shule wawe na tajiriba ya ualimu tu, asilimia 34 inahitaji tajiriba ya ualimu na usimamizi, asilimia 11 huitisha tajiriba yoyote inayohusiana katika elimu, asilimia 2 huitisha tajiriba katika nafasi nyingine yoyote ya usimamizi au uongozi na asilimia 7 haina masharti yoyote mahususi ya tajiriba. Nchini Ethiopia, asilimia 53 ya viongozi wa shule hawakuwa na tajiriba ya usimamizi kabla ya kuteuliwa.


**Historia ya elimu na tajiriba ya wakuu wa shule inatofautiana katika nchi mbalimbali, ikionyesha kiwango cha kuhitimu katika elimu, demografia na sera za kuajiri.** Katika mifumo 39 ya elimu liyoshiriki katika Utafiti wa Kimatifa wa Mienendo katika Hisabati na Sayansi (TIMSS) wa mwaka wa 2019, miongoni mwa wanafunzi wa sekondari za ngazi ya chini, asilimia 2 walikuwa na mkuu wa shule ambaye hakuwa na shahada ya kwanza, asilimia 43 walikuwa na mkuu wa shule mwenye shahada ya kwanza na asilimia 55 walikuwa na mkuu wa shule mwenye shahada za juu. Katika utafiti wa TALIS wa 2018, wakuu wa shule za sekondari za ngazi ya chini walikuwa na hatamu za wastani wa miaka kumi, saba kati ya hiyo ikiwa katika shule ya sasa. Huko Japan na katika Jamhuri ya Korea, wastani wa hatamu ulikuwa chini ya miaka tano, ilhali nchini Colombia na katika nchi za Baltiki ulikuwa miaka 13 hadi 16. Wakuu wa shule nchini Australia, New Zealand na Singapuri walikuwa na tajiriba ya awali maradufu (miaka kumi) katika kazi nyingine za usimamizi wa shule ikilinganishwa na nchi zingine (miaka tano).

**Hakuna uanuai wa kutosha katika nafasi za uongozi za shule.** Miongoni mwa kama nchi 40 zenye data katika elimu ya msingi na ya sekondari, kwa wastani, sehemu ya wakuu wa shule wanawake ilikuwa chini kwa angalau pointi 20 za asilimia ikilinganishwa na sehemu ya wastani ya walimu wanawake. Katika shule za msingi na sekondari za ngazi ya chini, pengo hilo lilikuwa angalau pointi 30 za asilimia huko Japan, Jamhuri ya Korea, Afrika Kusini, Türkiye na Viet Nam. Baadhi ya nchi zimeweka viwango vya uwiano wa jinsia, ikiwemo Rwanda ambapo asilimia 30 ya nafasi za uongozi imetengewa wanawake. Katika nchi nyingi, kuongezeka kwa uanuai katika jumuiya za shule hakujaendana na uanuai katika uongozi wa elimu. Nchini Uingereza, wanafunzi Weusi wanajumuisha asilimia 32 ya wanafunzi wanaosajiliwa katika shule za msingi na za sekondari, huku wanafunzi wa Asia na wa jamii ndogo ndogo wakijumuisha asilimia 29, lakini ni asilimia mbili tu ya wakuu wa shule walikuwa wa vikundi hivi katika mwaka wa 2020.

**MCHORO WA 2:**

**Ni wakuu wa shule wachache huanza hatamu yao ya uongozi wakiwa wamefanya kozi ya usimamizi wa shule**

*Asilimia ya wakuu wa shule wa sekondari za ngazi ya chini ambao wamepata mafunzo au kozi ya usimamizi wa shule au mafunzo ya wakuu wa shule, kulingana na wakati, nchi zilizochaguliwa zenye mapato ya wastani na ya juu, 2018*




*GEM StatLink:* https://bit.ly/GEM2024_Summary_fig2

*Chanzo:* OECD (2019).

**Kiwango cha matayarisho ya wakuu wa shule kabla ya kuteuliwa unatofautiana kati ya nchi.** Viongozi wa shule ambao wamepata mafunzo ya kuwa walimu bora tu huwa hawajatayarishwa vya kutosha kwa wajibu wao. Katika utafiti wa TALIS wa mwaka wa 2018, asilimia 88 ya wakuu wa shule wa sekondari za ngazi ya chini walikuwa wamewahi kukamilisha mafunzo au kozi iliyojumuisha kipengele cha usimamizi wa shule au mafunzo ya wakuu wa shule wakati mmoja katika kazi yao. Lakini ni asilimia 30 tu ya wakuu wa shule walikuwa wamekamilisha mafunzo au kozi kabla ya kuchukua nyadhifa zao, asilimia 24 walifanya hivyo kabla na baada ya kuchukua nyadhifa zao, na asilimia 34 walifanya hivyo baada ya kuchukua nyadhifa zao tu. Bulgaria, Meksiko na Uholanzi zilikuwa miongoni mwa nchi ambapo chini ya mkuu mmoja wa shule kati ya kila tano alikuwa amepata mafunzo au kufaya kozi ya usimamizi wa shule kabla ya kuchukua wadhifa huo **(Mchoro wa 2)**. Miongoni mwa wakuu hao wa shule, asilimia 15 walitaja kuwa kuna haja kubwa ya mafunzo kuhusu usawa na uanuai, asilimia 28 walitaja haja ya mafunzo ya teknolojia na asilimia 28 wakataja haja ya mafunzo ya ushirikiano wa walimu.


**Mipango ya kutayarisha na kuendeleza viongozi inatofautiana katika nchi mbalimbali.** Kuna mafunzo ya kabla ya kuteuliwa kwa wenye azma ya kuwa wakuu wa shule, mafunzo ya mapema na ya kuelekeza wakuu wapya wa shule, na mafunzo ya mara kwa mara ya maendeleo ya kitaaluma kwa wale ambao tayari wanashikilia wadhifa huo, ikiwa ni pamoja na mafunzo ya uzoefu wa hali halisi. Nchini China, wakuu wapya wa shule sharti wahudhurie na wakamilishe mafunzo ya saa 300, huku kila mkuu wa shule anayehudumu sharti akamilishe angalau saa 360 za mafunzo kila miaka mitano katika taasisi za mafunzo zilizoidhinishwa.

**Matayarisho mara nyingi hayapiti kiwango cha ujuzi wa kinadharia.** Kuna manufaa zaidi wakati matayarisho yanajumuisha mafunzo ya uzoefu wa kazi, ulezi na uzoefu wa hali halisi katika shule. Nchini Singapuri, kama sehemu ya Mpango wa Viongozi katika Elimu, wakuu wote wapya wa shule hupata mafunzo ya kuwaelekeza ya Mpango wa Ulezi katika mwaka wao wa kwanza wa kuhudumu. Nchini Kambodia, mtalaa wa mafunzo ya uongozi unajumuisha

warsha za maendeleo ya kitaaluma, kozi za uzoefu na miradi ya kuimarisha shule, ukilingana na viwango vilivyowekewa wakuu wa shule.

**Nchi zinaendelea kuweka kipaumbele kwenye mafunzo ya kazini kuliko mafunzo ya kabla ya kuhudumu na ya kuwaelekeza wanaoingia katika nyadhifa.** Duniani, asilimia 88 ya nchi zimeeleza mafunzo ya mara kwa mara kazini ya maendeleo ya kitaaluma kwa wakuu wa shule katika sheria au sera zao, lakini ni asilimia 60 pekee zinataja mafunzo ya kabla ya kuteuliwa na asilimia 31 zinataja mafunzo ya kuelekeza wakuu wapya wa shule. Nchini India, Sera ya Taifa ya Elimu ya mwaka wa 2020 inaifanya sharti kwa

**MCHORO WA 3:**
**Ni humusi tu ya mipango ya matayarisho na mafunzo kwa wakuu wa shule inashughulikia vipengele vyote vinne vya uongozi**
*Asilimia ya mipango ya matayarisho na mafunzo kwa wakuu wa shule, kulingana na kipengele kinachozingatiwa, nchi zilizochaguliwa, 2024*




*GEM StatLink:* https://bit.ly/GEM2024_Summary_fig3
*Chanzo*: Uchambuzi wa timu ya Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu kulingana na maelezo ya nchi katika PEER.

wakuu wa shule kukamilisha angalau saa 50 za mafunzo ya maendeleo ya taaluma kila mwaka. Lakini katika utafiti wa TALIS wa mwaka wa 2018, asilimia 46 ya wakuu wa shule za sekondari za ngazi ya chini waliripoti mgongano kati ya kujiendeleza kitaaluma na kazi (asilimia 82 nchini Japan), asilimia 36 walitaja sababu kuwa ukosefu wa vichochezi (asilimia 84 nchini Saudia) na asilimia 32 wakataja masuala ya gharama ya mafunzo (asilimia 68 nchini Kolombia).

**Kuna ukosefu dhahiri wa uwiano mzuri katika ushughulikiaji wa masuala muhimu ya uongozi.** Taarifa kuhusu mipango 142 ya matayarisho na mafunzo kwa wakuu wa shule kutoka nchi 92 zinatathmini kiwango ambacho mipango hiyo inazingatia vipengele vinne muhimu vya uongozi: kuweka maono (asilimia 42) na kuzingatia masomo (asilimia 47) ndivyo vipengele vilivyoshughulikiwa sana, vikifuatiwa na kuendeleza wafanyakazi (asilimia 31) na kukuza ushirikiano (asilimia 29). Ni asilimia 18 tu ya mipango yote ya mafunzo ilishughulikia vipengele vyote vinne. Mafunzo ya mara kwa mara kazini ya maendeleo ya taaluma yana uwezekano mkubwa zaidi wa kushughulikia vipengele vinne vya uongozi kuliko mafunzo ya kabla ya kuteuliwa. Uchambuzi unadokeza kuwa angalau nusu ya mipango hiyo ya mafunzo inazingatia uongozi wa kimageuzi na elekezi, ilhali uongozi wa pamoja hausisitizwi sana **(Mchoro wa 3)**.

**Mipango bora ya mafunzo ya uongozi huimarisha matokeo ya elimu.** Nchini Argentina, wakuu wa shule za msingi ambao walipokea vidokezo kutokana uchunguzi na wakaelewa jinsi ya kuvitumia walisaidia shule zao kupata matokeo bora kuliko shule ambazo hazikupata vidokezo hivi kwa pointi 0.33 za mkengeuko wastani katika alama za hisabati na pointi 0.36 za mkengeuko wastani katika alama za kusoma. Nchini Guatemala, mpango wa mafunzo kwa wakuu wa shule ulisaidia kupunguza kiwango cha wanafunzi kuacha shule kwa asilimia 4 kwa gharama ya chini ya Dola 3 za Marekani kwa kila mwanafunzi.

**Uthibitishaji wa kuhitimu kwa wakuu wa shule unaweza kuimarisha uongozi bora.** Uthibitishaji wa kuhitimu ni utaratibu rasmi ambapo maarifa na ujuzi wa wakuu wa shule unaweza kutathminiwa, kuthibitishwa na kutambuliwa, na ni hatua muhimu ya utaalamishaji. Katika utafiti wa TIMMS wa 2019, asilimia 68 ya wanafunzi wa darasa la nne na asilimia 71 ya wanafunzi wa darasa la nane walisomea shule ambapo wakuu wa shule walikuwa na cheti au leseni ya uongozi wa shule. Katika Jamhuri ya Kiislamu ya Irani, Wizara ya Elimu hutoa vyeti vinavyotumika kwa miaka tano kulingana na tathmini za ustadi, ambazo hudhihirisha uwezo wa kushikilia nafasi ya usimamizi katika shule. Nchini Ufilipino, manaibu wakuu wa shule na wenye azma ya kuwa wakuu wa shule sharti wapite Mtihani wa Kitaifa wa Kuhitimu wa Wakuu wa Shule. Nchini Afrika Kusini, Idara ya Elimu iliidhinisha Vigezo vya Kitaifa vya Kuhitimu kwa Viongozi wa Shule, kigezo cha lazima cha kuhitimu kitaaluma kilichobuniwa kwa ushirikiano na vyuo 14, vyama, Muungano wa Wakuu wa Shule wa Afrika Kusini na mashirika mbalimbali yasiyo ya serikali .

**Mazingira ya kazi ya wakuu wa shule yanachangia pakubwa kiwango cha kudumu na kuridhika kazini.** Nchini Australia, wakuu wa shule waliripoti kufanya kazi

kwa karibu saa 60 kwa wiki, huku vyanzo viwili vikuu vya msongo vikiwa wingi tu wa kazi na ukosefu wa muda wa kuzingatia ufundishaji na ujifunzaji. Nchini Ugiriki, wakuu wa shule waliripoti kuzongwa na kazi za kiusimamizi, iwe ni kusimamia mishahara ya walimu mbadala au kushughulikia ukarabati wa shule, zote ambazo hudunisha majukumu yao ya uongozi elekezi. Finland imeratibu michakato ya usimamizi kwa ajili wa wakuu wa shule, ikiwawezesha kuzingatia zaidi uongozi elekezi na hivyo imeimarisha kuridhika kwao kazini na matokeo ya wanafunzi.

**Kiwango cha kuridhika kazini kiko juu, lakini masuala ya msongo na uchovu kupita kiasi bado yanajitokeza sana.** Kwa mujibu wa utafiti wa TALIS wa 2018, asilimia 79 hivi ya wakuu wa shule za sekondari za ngazi ya chini katika mifumo 48 ya shule walikubaliana au kukubaliana kabisa na kauli kwamba faida za taaluma yao zinazidi kabisa hasara, vivyo hivyo, asilimia 86 na kauli kwamba, kama wangeweza kuamua tena, bado wangechagua kazi/nafasi hii. Data ya kuondoka kazini bado ni haba. Nchini Marekani, hakuna ushahidi unaodokezea ongezeko la kiwango cha kuondoka kazini. Katika mwaka wa 2021–2022, ilikadiriwa kuwa asilimia 80 ya wakuu wa shule walisalia katika shule ile ile, asilimia 6 walihamia shule nyingine na asilimia 11 waliacha taaluma hii, kiwango ambacho kimsingi hakikubadilika ikilinganishwa na juhudi za awali za ukusanyaji wa data katika miaka ya 2012–2013 na 2016–2017. Nchini Uswidi, uchambuzi wa data ya usimamizi kati ya mwaka wa 1980 na 2017 inaashiria kwamba kiwango cha kuhama kiliongezeka kidogo katika kipindi hicho lakini haikumaanisha moja kwa moja kwamba sababu ni kuzorota kwa mazingira ya kazi. Hata hivyo, msongo na uchovu kupita kiasi ni matatizo yanayojitokeza sana. Janga la COVID-19 liliwaweka wakuu wa shule katika hali ya shinikizo kubwa. Nchini Australia, asilimia 48 ya wakuu wa shule walionyesha "ishara za tahadhari" kuhusiana na afya ya akili katika mwaka wa 2022, hali inayoashiria kiwango cha juu cha msongo.

**Mifumo ya tathmini inaweza kuimarisha ufanisi wa wakuu wa shule.** Duniani, asilimia 78 ya nchi zina mifumo ya tathmini za kazi kwa ajili ya wakuu wa shule. Lakini mifumo ya tathmini za kazi huenda isisaidie maendeleo ya wakuu wa shule kikamilifu. Katika asilimia 39 ya nchi, tathmini zinahusishwa na lawama na adhabu. Nchini Chile, wakuu wa shule hutia sahihi mkataba wa utendakazi wa miaka tano na wanawajibika kutimiza malengo mahususi yanayohusiana na usajili, uhudhuriaji na mafanikio. Mikataba ya utendakazi hufungamana moja kwa moja na adhabu, ikiwa ni pamoja na mkataba kufutiliwa mbali mapema ikiwa manispaa itaonelea kwamba utendakazi wa mkuu wa shule hauridhishi. Katika Jamhuri ya Moldova, mkataba wa mkurugenzi unaweza kufutiliwa mbali endapo ataendelea kupewa alama za kutoridhisha katika tathmini za nje. Kinyume chake, viongozi wa shule nchini Singapuri hutathminiwa kulingana na mfumo wa taratibu unaohusishwa na maendeleo ya kikazi, huku wakuu wa shule wanaofanya vyema wakipiga hatua kuchukua majukumu makubwa zaidi ya uongozi.

### UONGOZI WA PAMOJA SHULENI:

**Wakuu wa shule wanapogawa majukumu ya uongozi kwa wafanyakazi, wanafunzi, wazazi na jamii, inaweza kukuza ubunifu, ujumuifu na kuimarisha mazingira ya elimu.** Licha ya uwezekano huu, uongozi wa shule mara nyingi husalia wa urasimu na hupunguza kuhusika kwa wadau. Wakuu wa shule hawapokei matayarisho ya kutosha ya kukuza ushirikiano. Walimu wanahitaji mafunzo ya uongozi na uhuru wa kufanya maamuzi. Ushiriki wa wanafunzi haujakita mizizi. Wazazi na jamii hukabiliana na vikwazo vya kushiriki kwao.

**Manaibu wakuu wa shule wanaweza kusaidia kubainisha maono ya shule, kusimamia michakato na kubuni mikakati ya ufunzaji.** Usaidizi bora kwa manaibu wakuu wa shule unajumuisha mamlaka bayana, ulezi wenye mpangilio na mafunzo ya mara kwa mara. Hata hivyo, bado hakuna ubayana kuhusu wajibu huo na manaibu wakuu wa shule wanaweza kukosa muda wa kuchangia katika uongozi. Uwakilishi wa manaibu wakuu wa shule katika timu za usimamizi unatofautiana ulimwenguni, Japan na Singapore zikiwa na uwakilishi kamili, huku Colombia ikiwa na uwakilishi wa asilimia 21 na Croatia asilimia 27. Huko Hong Kong, China, manaibu wakuu wa shule 300 waliripoti tofauti kubwa kati ya muda waliotengea sehemu mbalimbali za kazi na fikira zao kuhusu umuhimu wa kazi hizo.

**Walimu wanaoshikilia nyadhifa za kati za uongozi, kama vile waratibu wa masomo na wakuu wa mtaala, wana jukumu muhimu sana katika kuelekeza kufundisha na kujifunza.** Hata hivyo, walimu walio katika nyadhifa hizi mara nyingi huwa hawana mafunzo ya usimamizi na ujuzi wa mahusiano. Wakati mwingine majukumu yao si bayana na vichocheo vya kifedha havitoshi. Kwa mfano, nchi za Ugiriki na Ureno hazitoi malipo ya ziada kwa kazi za usimamizi. Kuhusika kwa walimu viongozi katika timu za usimamizi wa shule pia unatofautiana sana: nchini Israel na Kazakhstan, wakuu wa idara wapo katika zaidi ya asilimia 85 ya timu, huku nchini Ufaransa na Saudia, ushiriki wao uko chini ya asilimia 10. Utafiti wa Kimataifa wa Uongozi wa Walimu unapendekeza vipengele vya uongozi vijumuishwe katika mafunzo ya awali ya walimu ili waelewe uhusiano kati ya uongozi wa walimu, utamaduni wa shule na ufundishaji.

**Walimu wanaweza kuongoza vyema hata bila nyadhifa rasmi za uongozi.** Kuwalea wenzao, kukuza ubunifu na kuelekeza utamaduni wa shule ni michango muhimu. Huko Delhi, nchini India, walimu mwanzoni walikuwa na dukuduku kuhusu kusimamiwa, lakini hatimaye waliwaamini walezi na waratibu wao na kutambua jukumu la viongozi wa kati. Walimu walio katika nyadhifa za uongozi pia huunganisha shule na familia na wanafunzi. Nchini New Zealand, wanatoa usaidizi kwa wanafunzi ambao lugha yao ya nyumbani si Kiingereza kwa kujenga uhusiano na familia zao na kwa kuandaa hafla zinazokuza kujiamini kwa wanafunzi na fahari yao kwa lugha na utamaduni wao.

**Wafanyakazi wasaidizi wanaweza kuonyesha uongozi kwa kutambua na kukabiliana na vikwazo vya elimu na kisha kusaidia kuelekeza mikakati ya elimu.** Katika jimbo la Marekani la New Jersey, wakuu wa shule walitegemea ushauri wa pamoja wa wanasaikolojia wa shule, wataalamu wa ufundishaji na wasimamizi wa wilaya kufanya maamuzi yenye maarifa kuhusu elimu jumuifu. Wauguzi wa shule pia huongoza juhudi za afya kama vile kampeni za chanjo, na husaidia kuboresha matokeo ya wanafunzi kama vile ulaji wa lishe bora zaidi na kupungua kwa wasiwasi.

**Wanafunzi wanaweza kutoa uongozi rasmi na usio rasmi.** Nyadhifa rasmi, kama vile kwenye mabaraza ya wanafunzi na kamati za usimamizi, huathiri sana mazingira ya elimu ya wanafunzi na ukuaji wao binafsi. Duniani, asilimia 57 ya nchi zimeweka sharti kwamba wanafunzi wawakilishwe kwenye bodi na halmashauri za shule. Ijapokuwa mabaraza ya wanafunzi kwa kawaida huchaguliwa kupitia kura, hayahusiki sana katika kufanya maamuzi na hili hatimaye hudunisha mamlaka ya wanafunzi. Nchini Poland, utafiti wa mabaraza ya shule za sekondari ulipata kwamba wasimamizi wengi wa mabaraza waliwalazimishia wanafunzi mwelekeo na hivyo kuzima shauku ya kushiriki kikamilifu na kufanya maamuzi. Uongozi usio rasmi ni pamoja na mipango binafsi ya kusoma na mikutano ya walimu na wanafunzi. Baadhi ya serikali huanzisha kumbi wazi na kuwaalika wanafunzi watoe maoni yao kuhusu elimu, kama vile katika Safu ya Kujieleza ya Bodi Kuu ya Elimu ya Sekondari (CBSE) na Idara ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana nchini Afrika Kusini. Ijapokuwa ni jambo nadra na la majaribio, shule kama vile Mechai Pattana nchini Thailand zinawasaidia wanafunzi kuhusika pakubwa katika utawala wa shughuli zote za shule na zinakuza uongozi kupitia juhudi za kijasiriamali na huduma kwa jamii.

**Wazazi na wanajamii wenye motisha wanaweza kuelekeza shule kufikia malengo.** Kama wawakilishi katika kamati za usimamizi wa shule, wazazi na wanajamii hufanya uangalizi wa usimamizi wa shughuli, sera, bajeti na rasilimali za shule. Nchini Albania na Ecuador, wana ushawishi katika bajeti za shule na tathmini za walimu, ilhali nchini Kenya, wao hufanya uangalizi wa taratibu na uajiri wa wafanyakazi. Vyama vya wazazi na walimu hushughulikia masuala kama vile elimu ya wasichana huko India, ujumuishaji wa wenye elemavu nchini Sudan Kusini na huwasaidia wanafunzi walio katika hali ngumu nchini Viet Nam. Wakuu wa Shule hukuza kushiriki kwa wazazi kupitia mawasiliano ya mara kwa mara, huku asilimia 64 ya shule zikiwataka wajulishe wazazi kuhusu matokeo ya shule na ya wanafunzi. Duniani, asilimia 83 ya nchi zimeifanya kwa wazazi kushiriki katika utawala wa shule, ijapokuwa asilimia 62 zinajumuisha wanajamii. Viwango vya kushiriki kwa wazazi vinaripotiwa kuwa juu katika nchi za Amerika ya Kilatini, kama vile Kolombia (asilimia 55), Jamhuri ya Dominika (asilimia 59) na El Salvador (asilimia 60). Katika hali halisi, uteuzi wa wanachama wa kamati za usimamizi na bodi za shule huathiriwa na mwingiliano wa jamii, hali ambayo inaweza kusababisha kutengwa kwa watu. Nchini Honduras, utafiti wa shule zinazosimamiwa na jamii ulipata kwamba wanasiasa kuwa na mamlaka ya kuteua watu katika vyeo kulidunisha uwazi na uwajibikaji.

## UONGOZI WA MIFUMO:

**Maafisa wa elimu katika ngazi za kati na za mashinani wanaweza kuwa viongozi wa mifumo.** Viongozi wa mifumo ni maafisa wa elimu ambao vitendo vyao hufanya zaidi ya kuhakikisha tu utii wa michakato ya usimamizi na taratibu za utawala walizoajiriwa kutekeleza tu. Katika kiwango cha kati, wanaweza kutumia fikra za kimkakati kutabiri mahitaji, kutafuta masuluhisho na kuleta sera na mageuzi. Kitika kiwango cha mashinani, ikitegemea mipangilio ya utawala, kama maafisa wa wilaya, wasimamizi au wakaguzi, wanaweza kufanya maamuzi kuhusu mgao wa rasilimali, usimamizi wa rasilimali na usaidizi kwa walimu.

**Upatano kati ya uundaji na utekelezaji wa sera ni ishara ya uongozi.** Katika mkoa wa Canada wa Ontario, utafiti wa zaidi ya viongozi 2,000 wa wilaya na wa shule katika wilaya 45 za shule ulionyesha kwamba kujifunza kwa wanafunzi kuliathiriwa na matumizi ya uongozi wa kimfumo, kama unavyodhihirika katika maoni, azma na malengo, upatano wa mpango wa mafunzo na malengo hayo, utekelezaji madhubuti wa mipango na matumizi ya data. Nyadhifa za uongozi za wilaya ziliathiri elimu zaidi ya aina na ubora wa uongozi wa shule. Jimbo la Meksiko la Puebla lilibadilisha wajibu na uwezo wa wasimamizi ambao kazi yao ilikuwa inakomea masuala ya utiifu tu. Nchini Norwe, maafisa wa elimu wa manispaa waliripoti kuchangia katika ujumuifu kwa kuimarisha uhuru wa walimu na ustadi wa kufundisha.

**Viongozi wa mitaa wana uwezekano mkubwa zaidi wa kuchangia katika kuboresha matokeo ya elimu wanapokuwa na mamlaka na uwezo wa kuunda na kutekeleza sera.** Nchini Kolombia, manispaa kubwa zenye

majukumu kamili ya kuajiri, kufunza na kuweka walimu kazini; miundomsingi ya shule; nyenzo na usafiri wa shule zimehusishwa na sehemu ndogo zaidi ya wanafunzi wenye matokeo mabaya katika masomo ya Kihispania na Hisabati katika madarasa ya 3, 5 na 9. Lakini mageuzi ya ugatuzi nchini Moroko yaliyolenga kuwapa watawala wa eneo uhuru mwingi wa usimamizi na kifedha haukuimarisha matokeo, kwa kiasi fulani ikiwa ni kwa sababu ya uwezo mdogo mashinani na kwa upande mwingine ni kwa sababu mamlaka ya kati yalidumisha udhibiti wa kufanya maamuzi.

**Uongozi wa mifumo unaweza kukwamishwa na ukosefu wa mwelekeo bayana na wa motisha ya kutenda ili kutimiza lengo la pamoja.** Utafiti wa maafisa wa elimu wa kitaifa na wa wilaya nchini Brazil, Jamhuri ya Dominika, Guatemala na Peru ulionyesha kwamba walishindwa katambua majukumu manne kati ya matano ambayo wanatarajiwa kutekeleza kwa mujibu kwa sheria. Pia walidai kuwajibika kwa jukumu moja katika ya kila matatu yaliyokabidhiwa viwango vingine vya serikali. Ukosefu huo wa kuelewa wajibu wao ulikuwa na uhusiano hasi na matokeo ya mafunzo katika shule za wilaya zao.

**Wajibu wa mageuzi mara nyingi haupewi wale wanaopaswa kuyatekeleza.** Baadhi ya nchi huweka mipango mikubwa ya mageuzi lakini hukabidhi jukumu la utekelezaji kwa idara nyingine au vitengo vya utekelezaji ambavyo vina wasimamizi wenye uhuru zaidi katika kufanya maamuzi. Waelekezi na washauri wa nje wanaweza kubainisha viwango, kutathmini mifumo na maendeleo ya sera na kutoa ushauri kuhusu mageuzi. Kwa mfano, nchini Malaysia, Kitengo cha Usimamizi wa Utendakazi na Utekelezaji kilikuza mashauriano mpana na ya mara kwa mara na ushirikiano wa karibu kati ya viwango vya kati na vya eneo katika kupatia sera kipaumbele, kuweka malengo na kufuatilia utekelezaji. Lakini si kila mara vitengo vya utekelezaji vimeleta matokeo yaliyotarajiwa, kimsingi ikiwa ni kwa sababu suala la kubadilisha maadili, mitazamo na uwezo wa maafisa wa elimu halijazingatiwa sana, kama ilivyokuwa katika mageuzi ya serikali ya mtaa ya mwaka wa 2019 katika mkoa wa Punjab huko Pakistan.

**Viongozi wa mifumo wanastahili kuwa viongozi wa kuelekeza.** Viongozi wa mifuno wanaweza kusaidia kudumisha kuzingatiwa kwa matokeo ya mafunzo kwa kufuatilia data ili kuelewa mahitaji, kuwezesha maendeleo ya kitaaluma na kutoa usaidizi wa ufundishaji. Lakini changamoto moja kubwa ni kwamba wafanyakazi wa serikali walioajiriwa katika nyadhifa kama hizo huenda wasiwe wametayarishwa kwa masuala ya kitaaluma ya kazi yao au huenda hata hawafahamu wajibu wanaokusudiwa. Nchini Ghana, utafiti wa ofisi 174 za elimu ya wilaya uliofanywa kulingana na vigezo vya Utafiti wa Usimamizi Duniani ulionyesha kwamba maafisa wa wilaya wana uwezekano mdogo wa kuweka mipango kimkakati na kufuatilia, kwa sababu dta hukusanywa lakini haipitiwi na kutumiwa kila wakati.

**Wakaguzi wa shule wanaweza kuwa viongozi wa mifumo.** Wakaguzi hushauri, husaidia na kufadhili wakuu wa shule kadhaa kwa wakati mmoja. Katika Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, idadi za ziara za kukagua shule na jinsi ziara hizo zilivyofanywa ilikuwa mojawapo ya vishawishi muhimu zaidi vya kuimarika kwa ujifunzaji. Lakini kwa jumla, ukaguzi ungali unakomea kutoa ripoti huku ukiwa na athari ndogo kwenye matokeo ya shule. Utafiti katika mkoa wa Shandong nchini China ulionyesha kwamba kuimarika kwa shule kulieleweka kama kutii viwango, kanuni na sera za kitaifa, na wakaguzi hawakushughulika na katambua michakato na matokeo ya shule ya kuboreshwa.

**Si kila mara viongozi wa mifumo wanachaguliwa kuhudumu katika nafasi hii.** Ni asilimia 12 ya maafisa wa mipango nchini Ethiopia na chini ya asilimia 10 nchini Guinea walikuwa na tajiriba ya elimu katika upangaji na usimamizi. Huko Bangladesh, India na Pakistan, wafanyakazi wa serikali huajiriwa kufanya kazi maisha yao yote popote katika utawala wa umma na ujuzi wao mara nyingi hauhusiani na matakwa ya kiufundi ya nyadhifa za zamu wanazopewa. Uaminifu kwa kikundi ambacho mfanyakazi wa serikali anatokea husisitizwa zaidi ya ustahilifu. Kinyume na hayo, wafanyakazi wote wa serikali katika Jamhuri ya Korea huteuliwa kwa msingi wa tathmini ya lazima ya uongozi. Kundi la wakaguzi waliohitimu hutathmini uwezo wa kuongoza wa mtafutakazi kupitia vielelezo vya matatizo ya sera na usimamizi.

**Viongozi wa mifumo wanaweza kufunzwa kutekeleza majukumu ya uongozi.** Nafasi za maendeleo ya kitaaluma zinaweza kuziba pengo katika vipengele vyote vya uongozi. Nchini Brazili, mpango wa Jovem de Futuro umetoa mafunzo kwa wakurugenzi, wakaguzi na wakurugenzi wa maeneo kuhusu jinsi ya kutambua malengo yanayowazingatia wanafunzi na kuhakikisha upatano katika utekelezaji. Katika hali fulani, watoa huduma wa kibinafsi huziba mapengo ya mafunzo ya uongozi. Kampuni ya Edvolution Enterprise kufikia sasa imetoa mafunzo kwa maafisa 176 wa elimu ya wilaya kwa ushirikiano na Wizara ya Elimu ya Malaysia.

## UONGOZI WA KISIASA


**Wahusika mbalimbali hutekeleza wajibu muhimu katika michakato ya kisiasa na ya kijamii ili kuelekeza malengo ya elimu na kuathiri maamuzi.** Viongozi wa kisiasa wenye maono wanaweza kuweka kipaumbele katika elimu na kujenga miungano ya utendaji. Wahusika wasio wa serikali wanaweza kuelekeza serikali kwenye maono yao ya elimu na kuwataka watawala kuwajibika. Hata hivyo, motisha na

maslahi ya wahusika hawa huenda yasioane kikamilifu na lengo la kuboresha elimu. Isitoshe, vitendo vyao vinaweza kubanwa na ukosefu wa tajiriba, rasilimali na mazingira ya kuwawezesha kutoa uongozi.

**Elimu inajitokeza sana katika ajenda za kitaifa za kisiasa.** Mara nyingi elimu husisitizwa katika mipango ya maendeleo ya kitaifa. Serikali pia hutumia mifumo ya elimu kuendeleza maono fulani ya uraia na utambulisho wa kitaifa. Utafiti wa mwaka wa 2020 wa zaidi ya maafisa wakuu 900 wa serikali za nchi 35 zenye mapato ya chini na ya wastani ulipata kwamba waliweka mafunzo ya utamaduni kama matokeo ya kipaumbele zaidi, ikifuatiwa na ukamilishaji wa elimu ya sekondari, kisha uwezo wa msingi wa kusoma, kuandika na hisabati. Kinachotiliwa mkazo na mtalaa – yaani kusisitizwa kwa maudhui na ishaa za uzalendo – kinaweza kutofautiana kulingana na aina ya utawala wa kisiasa. Mabadiliko ya serikali yanapohusishwa na mabadiliko makubwa ya itikadi, elimu inaweza kuwa uwanja mkuu wa mapambano.

**Vitendo katika elimu mara nyingi huelekezwa na faida za uchaguzi badala ya masuala ya muda mrefu.** Ingawa serikali nyingi serikali nyingi hujaribu kuelekeza elimu ilingane na maono yao ya maendeleo ya kitaifa, maamuzi ya elimu mara nyingi hutokana na siasa za uchaguzi, ikiwa ni pamoja na upendeleo na mabadilishano kati ya vyama na wapiga kura. Katika mwaka wa 2021, asilimia 29 ya nchi zilikuwa na uwezekano wa kutumia maoni ya kisiasa kama msingi wa maamuzi yao ya kuajiri au kufuta kazi mara nyingi au karibu kila wakati. Uhusiano wa karibu wa kisiasa unaweza kuleta madhara kwa matokeo ya elimu. Nchini Kenya, upendeleo wa kikabila katika elimu umesababisha ongezeko la idadi ya shule na hivyo miaka mingi zaidi ya kumaliza shule kwa wale wa kabila moja na rais au waziri wa elimu.

**MCHORO WA 4:**
**Asilimia 51 ya mawaziri wa elimu huwa wameondoka kwenye wadhifa huo ndani ya muda wa miaka miwili tangu kuteuliwa**
*Uwezekano kwamba waziri wa elimu angali kwenye wadhifa huo, kulingana na muda tangu kuteuliwa*




*Zingatia:* Uchambuzi huu unazingatia kipindi kati ya tarehe 1 Januari 2010 na tarehe 31 Desemba 2023 na unajumuisha mawaziri 1,412 wa elimu kutoka mifumo 211 ya elimu.
*GEM StatLink:* https://bit.ly/GEM2024_Summary_fig4
*Chanzo*: Uchambuzi wa timu ya Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu.

**Wanasiasa wanahitaji muda, usaidizi na motisha ili waongoze.** Mawaziri huweka uwiano kati ya matakwa mengi katika hatamu fupi. Uchambuzi kutokana na hifadhidata ya mawaziri 1,412 wa elimu tangu mwaka wa 2010 uliotayarishwa kwa ajili ya ripoti hii unaonyesha kwamba kwa wastani, waziri ana miaka 53, ana elimu ya juu (asilimia 72 wana shahada za juu) na ni mwanaume (asilimia 73). Kama asilimia 23 wana tajiriba ya awali ya kufunza katika shule za msingi na za sekondari. Wastani wa hatamu uko chini tu ya miaka miwili na miezi mitatu lakini iko chini zaidi, mwaka mmoja na miezi 11, kwa mawaziri katika nchi zilizo katika theluthi ya juu ya Kielezo cha Demokrasia Huru. Uwezekano wa kusalia kwenye wadhifa wa waziri wa elimu ni asilimia 79 katika mwaka wa kwanza, asilimia 49 katika mwaka wa pili na asilimia 33 katika mwaka wa tatu **(Mchoro wa 4).**

**Mawaziri wa elimu wametoa taarifa binafsi za waliyopitia na jinsi wanavyoleta mabadiliko.** Mawaziri nchini Canada na Denmark wametaja ukosefu wa matayarisho kwa kazi hiyo na ugumu wa kupata muda wa kutoa uongozi. Huko Peru, Sierra Leone na Delhi, India, mawaziri wa elimu walisisitiza jinsi kukuza miungani, kudhibiti mahusiano na mawasiliano yaliwasaidia kupata matekeo ya elimu waliyoyapata. Mawaziri pia hujitahidi kujifunza kutokana na mifano ya nchi zingine au kutumia mifano hiyo kuweka mfumo wa mageuzi yao.

**Watunga sheria wanaweza kuongoza kwa kutekeleza majukumu yao.** Wabunge wanaweza kuwa viongozi muhimu kwa kutekeleza majukumu muhimu ikiwa ni pamoja na kutunga sheria, utetezi, kuelekeza fedha za umma, kuchunguza vitendo vya serikali na kuwakilisha wakazi wa maeneo yao. Lakini wapiga kura wakati mwingine huwatathmini wabunge wao kwa misingi ya huduma ya moja kwa moja katika eneobunge. Nchini Kenya, mapendeleo haya ya wapiga kura yalisababisha kazi ya utungaji sera kutozingatiwa sana. Jinsia ya wabunge imedhihirishwa kuwa na athari katika sera, juhudi na matokeo ya elimu. Uchambuzi wa nchi 19 za OECD kati ya mwaka wa 1960 na 2015 ulionyesha kwamba kuongeza sehemu ya wabunge wanawake kwa pointi moja ya asilimia kuliongeza matumizi ya serikali katika elimu kama sehemu ya Pato la Taifa kwa pointi 0.04 za asilimia.

**Vyama vya walimu vinaweza kuleta mabadiliko lakini mara nyingi huonyeshwa kama vinapinga mabadiliko.** Vyama vya walimu huathiri sera za elimu kupitia utetezi, majadiliano ya pamoja na migomo. Kama kikundi kikubwa zaidi cha kitaaluma cha wafanyakazi wa serikali, wanaweza pia kuathiri uchaguzi. Kazi ya kuboresha ufundishaji na ujifunzaji inahitaji ushirikiano na vyama vya walimu, kwa sababu ni walimu hutekeleza mageuzi na wanaweza kupunguza upinzani dhidi ya mageuzi hayo. Katika mwaka wa 2021, kama sehemu ya utafiti wa kimataifa wa wawakilishi 128 wa vyama, ni asilimia 37 tu waliripoti kwamba serikali hutaka ushauri wa vyama kuhusu sera za elimu mara nyingi au kila wakati. Upungufu mmoja ni kwamba katika baadhi ya nchi, kama vile Indonesia na Tunisia, vyama vina nafasi ndogo ya kuathiri sera kwa sababu vina uwezo duni wa kubuni mapendekezo madhubuti ya sera.

**Vyama vya wanafunzi vinaweza kuongoza mabadiliko ya elimu na ya kijamii.** Vyama vya wanafunzi hutumia utetezi wa kisiasa kutaka uwajibikaji katika elimu na jamii. Vyama vya wanafunzi vimetetea haki ya kupata elimu nafuu na kujumuishwa katika uwakilishi wa elimu ya juu. Uhusiano kati ya vyama vya wanafunzi na serikali mara nyingi huwa ya uhasama, hasa wanafunzi watetezi wanapohusika au hata kuongoza harakati pana zaidi za kutaka demokrasia na mageuzi ya sera. Mara nyingi, harakati hizi hukomeshwa kwa fujo na viongozi wake huteswa kwa sababu za kisiasa na kuonyeshwa kama waasi. Hata hivyo, vitendo vyao vinaposababisha utawala kubadilishwa, viongozi wa wanafunzi wanaweza kutambuliwa kama mashujaa. Nchini Bangladesh na Chile, mavuguvugu ya wanafunzi yanaashiria tukio la kutajika ambapo uongozi wa wanafunzi umerasimishwa katika shughuli za serikali.

**Mashirika ya waajiri yanaweza kuelekeza sera za kuimarisha ustadi wa wafanyakazi.** Lakini uchambuzi wa mashirika 28 ya kitaifa ya uanachama wa waajiri na wanabiashara ulipata kwamba mengi hayakuweza kuongoza mifumo ya ujuzi kikamilifu. Nchini Marekani, ni asilimia tatu tu ya zaidi ya waangalizi 1,100 wa wilaya walikadiria viongozi wa biashara kuwa na ufahamu mwema wa elimu ya umma na asilimia 14 wakawakadiria kuwa wamepotoshwa. Jukumu moja la kawaida la uongozi la mashirika ya waajiri ni kuanzisha halmashauri za ujuzi katika sekta. Katika nchi zenye mifumo thabiti ya uwili kwa mafunzo ya kitaalamu, kama vile Ujerumani na Uswisi, biashara zimetoa mikataba ya uanagenzi, kuthibitisha ubora wa mafunzo na kuratibu mitihani.

**Watafiti hutoa uongozi kwa kushawishi mapendekezo ya sera.** Baadhi ya wahusika wana ushawishi mkubwa kwa kutoa uongozi wa maarifa, kutoa utafiti wa kufadhiliwa, kushiriki katika mijadala ya sera na kuhudumu katika nyadhifa za kamati za serikali, hali ambayo inaweza kuchangia katika utungaji sera unaotegemea ushahidi. Ijapokuwa utungaji sera unaotegemea ushahidi na uelewa wa mbinu zinazofaa katika elimu umezidi kusistizwa, pia kumekuwa na malalamiko kwamba mbinu hii imepunguza masuala ambayo yametafitiwa na swali la "kwa sababu gani" kitu kinafanya kazi linahitaji kuulizwa.

**Mashirika ya kimataifa hutekeleza wajibu wenye ushawishi mkubwa katika elimu.** Mashirika ya kimataifa yanaweza kutofautiana katika asili, uongozi, uanachama na hadhira yao, pamoja na katika aina za elimu yanayoendeleza. Licha ya hayo, yote yanaweza kutoa uongozi vivyo hivyo. Hata hivyo, yanakumbwa na changamoto. Yanahitaji kuwasilisha ujumbe dhahiri ili yawe ya maana. Mara nyingi, huwa yanashindana yenyewe kupata ushawishi wa kuvuta hadhira na ufadhili. Huwa yanapata mamlaka kutokana na amri, ufadhili na data. Shirika la OECD limekuwa na ushawishi katika uzalishaji na matumizi ya ushahidi, Benki ya Dunia katika ufadhili wake wa kifedha na wa kitaaluma, na UNESCO na sera zake zinazotegemea haki katika masuala kama vile ujumuifu. Lakini uwezo wa mashirika haya kuongoza unaweza kudunishwa na taratibu dhaifu za ndani, hatari ya kuvutwa na mitindo, uwekaji wa masharti, ushindani kupita kiasi na kuingiliwa na nchi wanachama.

**Uwajibikaji ni sehemu ya uongozi.** Asasi za raia mara nyingi huwa watetezi wakubwa wa kuzingatia masuala muhimu ya elimu. Juhudi za muda mrefu za kitaifa na kimataifa zimezingatia miundomsingi ya shule, utoaji wa vitabu vya kiada, upatikanaji wa data, msamaha wa madeni na mageuzi ya kodi. Mashirika yasiyo ya serikali yametetea haki ya kupata elimu na ujumuishaji wa vikundi ambavyo havijajumuishwa vya kutosha. Hata hivyo, jukumu lao katika uwajibikaji hutegemea uhusiano wao a serikali. Vyombo vya habari vina wajibu muhimu katika kutaka uwajibikaji kutoka kwa serikali na katika ufahamishaji. Uanahabari pelelezi unaweza kuangazia masuala yanayohitaji kufichuliwa, kama vile uhaba wa walimu, kashfa za dhuluma za kingono na ufujaji wa fedha. Uhuru kutoka kwa masilahi binafsi ni sharti kwa vyombo vya habari kuaminika na kutimiza wajibu wao wa uongozi, lakini kupungua kwa rasilimali kumedhoofisha uanahabari.

.

## MAPENDEKEZO

Uongozi ni muhimu katika elimu. Uongozi husaidia taasisi za elimu, mifumo ya elimu na jamii kuimarika. Viongozi huwafanyi kazi peke yao – huwa wanaitika wahusika wengine wanaosaidia kuathiri mfumo wa kisiasa: wabunge, watafiti, mashirika ya kimataifa, asasi za raia, vyama vya wafanyakazi, vyombo vya habari na wahusika wengine wengi. Wote hutoa uongozi, wakisaidia kuelekeza nchi kwenye malengo mahususi ya elimu na mapana zaidi ya kijamii. Baadhi ya wanasiasa, kwa mfano, wameweka kipaumbele kwa elimu bora ambayo ni jumuifu na yenye usawa katika nchi zao kupitia mageuzi yenye maono na utengaji wa rasilimali za kutosha. Lakini kabla ya kuangilia 'jinsi' uongozi unavyofanyika – na kuleta hatari ya uongozi wenyewe kuwa lengo – ni muhimu kuangalia 'nini' uongozi unapaswa kutimiza.

Uongozi hutekelezwa kwa njia nyingi na aina mbalimbali, ukizingatia tofauti katika miktadha, maadili, mitazamo na mashirika. Aina za matokeo ambayo viongozi huchangia ni nyingi mno, kiasi kwamba kuzingatia aina moja ili kurahisisha uchambuzi hudunisha athari kamili wa uongozi. Simulizi za viongozi bora zinatoa motisha lakini zinaweza tu kutoa mafunzo ya moja kwa moja kwa walio katika hali sawa. Changamoto ni kupata maarifa kutoka hadithi hizi za watu binafsi na kuzingatia taratibu za kitaasisi zinazoendeleza badala ya kuzimisha viongozi wenye vipawa wa aina na tajiriba zote, katika miktadha yote. Katika nchi nyingi, viongozi wa elimu mara nyingi hudhaniwa kuwa wasimamizi au mameneja tu. Hata hivyo, katika miaka ya hivi majuzi, baadhi ya nchi zimetambua upeo kamili wa kazi zao na kuweka misingi ya utaalamishaji wa kazi hizo. Nchi zingine zimechukua hatua za kuelekeza mbinu za uongozi, zikiwahimiza viongozi washirikiane zaidi na walio karibu nao. Hata hivyo, mabadiliko yanaweza kuchukua muda, hasa katika tamaduni na desturi za muda mrefu.

Mapendekezo manne ya ripoti hii yanazingatia hatua ambazo serikali zinaweza kuchukua ili kukuza uongozi katika elimu shuleni na katika utumishi wa serikali. Msingi wa mapendekezo haya ni vipengele vinne vya wajibu wa kiongozi wa elimu ambavyo ni vinawafaa katika kuongoza kwa ufanisi, iwe wanafanya kazi katika shule au ofisi ya elimu katika serikali: kama ilivyotangulizwa katika sehemu ya mwanzo ya muhtsari – kubainisha matarajio, kuzingatia ufunzaji, kukuza ushirikiano na kukuza uwezo. Vipengele hivi vinafaa kuwa msingi wa kujengea mikakati madhubuti ya kitaifa ya uongozi wa elimu inayotumika katika viwango vyote vya mfumo. Ili mfumo wa elimu ufanye kazi vyema, viongozi wa ngazi tofauti wanahitaji kufanya kazi kuelekea kutimiza malengo ya pamoja.

### PENDEKEZO LA 1. AMINI NA WEZESHA

*Kuza mazingira yanayowawezesha wakuu wa shule kuimarisha elimu*

Hakuna uongozi pasipo nafasi ya kufanya maamuzi. Viongozi wa elimu huchangia kuimarisha elimu katika hali na miktadha yote, lakini ushawishi wao huwa mkubwa zaidi kadri wanavyoaminiwa kutumia ujuzi wao. Hivyo basi, mifumo ya elimu inahitaji kuwawezesha wakuu wa shule kwa kuwapa uhuru wa kutosha wa kusimamia fedha na rasilimali watu na kufanya maamuzi yanayohusiana na ufundishaji na ujifunzaji.

Lakini haitoshi kuweka uhuru wa kufanya maamuzi bila mbinu za usaidizi. Serikali zinafaa kubainisha wazi mipaka ya mamlaka ya kufanya maamuzi ya viongozi wa shule. Zinahitaji kutoa rasilimali za kutosha kwa wakati, kwa usawa na kwa njia inayotabirika. Viongozi wa shule wanahitaji kuwajibika kwa serikali na jamii kwa ajili ya matumizi mema ya rasilimali hizi ili kutimiza malengo ya elimu yanayofikika. Serikali sharti zikuze uwezo wa viongozi wa kutumia rasilimali kwa ufanisi na uwezo wa serikali zenyewe wa kufuatilia shule na kutumia taarifa kwa ufanisi. Imani inafaa kuendelea kukuzwa kupitia mawasiliano ya maana na ya mara kwa mara. Serikali pia zinahitaji kufahamu na kulinda viongozi wa shule dhidi ya hatari zinazoweza kutokana na kuwa na uhuru zaidi.

### PENDEKEZO LA 2. TEUA, KUZA, TAMBUA

*Wekeza katika utaalamishaji wa wakuu wa shule*

***a. Teua wa wakuu wa shule wenye vipaji kupitia uteuzi jumuifu***

Mbinu za kuajiri zinahitaji kuwa jumuifu na kutambua kuwa uwezo wa kuongoza unaweza kupatikana ndani ya wale 'wasiojitanguliza na wapole, wanaoshangaa wanapotajwa kama viongozi bora'. Watu wenye vipaji huenda wakakatishwa tamaa ikiwa michakato si wazi na ya haki. Ijapokuwa kuna njia mbalimbali za kufikia wadhifa wa kiongozi wa shule, uwezekano wa mtu kuteuliwa kutoka nje ya kikundi cha walimu waliopo ni mdogo sana. Kwa hivyo, ni jambo la busara kujumuisha vipengele vya ukuzaji wa uongozi katika mafunzo ya awali ya ualimu. Utambuzi wa watu wenye vipaji na uwekaji wa mipango ya urithi wa uongozi unafaa kuwa sehemu muhimu ya mikakati ya kuajiri. Ni vizuri kutoa nyadhifa za usimamizi na uongozi mapema ikiwezekana. Hata hivyo, ni muhimu kuhakikisha kwamba mbinu hizi hazina ubaguzi, fikra potofu au upendeleo, na kuepuka miundo msonge, mitazamo finyu au ushawishi wa nje usio wa haki.

Vigezo vya kuajiri vinahitaji kubainishwa vyema, kuwa wazi na bila upendeleo ili kuhakikisha watafutakazi waliohitimu wana fursa sawa za kudhihirisha ujuzi wao anuai wa uongozi bila kujali usuli au jinsia yao. Siasa hazistahili kuchangia katika uteuzi wa viongozi wa shule. Ukosefu wa uanuai katika nyadhifa za uongozi ni tatizo katika michakato ya kufanya maamuzi ya elimu katika ngazi zote. Kwa sasa, nchi nane kati ya kila kumi hazijaweka mikakati ya kuhakikisha usawa katika uwakilishi. Michakato wazi ya uteuzi wa wafanyakazi inaweza kusaidia kupunguza pengo la uwakilishi katika nyadhifa za uongozi, lakini viwango vya uwiano vya muda huenda vikahitajika ambapo tatizo hili litaendelea kuwepo.

Si kila wakati walimu bora huwa wakuu bora wa shule – na kuna haja ya uangalifu ili wadhifa wa mkuu wa shule usidokezwe kuwa tuzo kwa walimu bora zaidi. Kwa upande mwingine, kuwa mwalimu bora ni muhimu ili kufanikiwa kama mkuu wa shule. Uchambuzi wa michakato ya uteuzi kwa ajili ya ripoti hii umeonyesha kwamba nchi tatu kati ya kila nne zinahitaji wakuu wa shule wawe walimu waliohitimu kikamilifu. Lakini ni kama 3 tu kati ya 10 hutaja tajiriba ya usimamizi kimahususi. Kwa hivyo vigezo vya uteuzi vinahitaji kupanuliwa na kufanywa anuai.

***b. Watayarishe, wafunze na wasaidie wakuu wa shule kuzingatia vipengele muhimu vya wadhifa wao.***

Uchambuzi wa kimataifa wa kozi za mafunzo kwa ajili ya ripoti huu, za kabla ya kuajiriwa na za kazini, unadokeza kwamba ni kama nusu tu ya kozi za mafunzo zinazingatia chochote kati ya vipengele vinne vya uongozi elekezi, matarajio na maono, ushirikiano na miungano, na maendeleo ya wafayakazi – na ni theluthi moja tu inazingatia vyote vinne. Mipango ya mafunzo inahitaji kuzingatia kila kipengele kati ya hivi vinne, lakini sanasana ni vya kiusomi na havitofautishi kati ya mahitaji yanayojitokeza katika awamu mbalimbali kazini.

Usaidizi wa aina fulani, kama vile mafunzo ya kuelekeza, ya kocha na ulezi, ni muhimu sana kwa mafanikio ya viongozi wapya na walio katika kipindi cha awali cha uongozi, ilhali umuhimu wake hudunishwa. Ni nchi tatu tu kati ya kila 10 zina kanuni za kutoa mafunzo kwa wakuu wapya wa shule baada ya kuteuliwa kwao. Mipango ya matayarisho inahitaji kujumuisha kipengele cha mazoezi au mafunzo ya hali halisi na kujumuisha waelekezi na walezi.

Mipango ya maendeleo ya kitaaluma yanastahili kuziba pengo, hasa kwa viongozi ambao mafunzo yao ya awali haikujumuisha vipengele vinne muhimu. Ujuzi unaoweza kukuzwa ni pamoja na stadi pana za kuchunguza, za kusikiliza, za kihisia na za uchambuzi. Mafunzo pia yanafaa kujumuisha vipaumbele vyovyote vya mageuzi vya serikali ili kusaidia utekelezaji wake, ikiwa ni pamoja na kuwafahamisha viongozi wa shule kuhusu sheria na kanuni muhimu, na kukuza ujuzi wa kiutendaji katika usimamizi wa data, fedha, rasilimali watu na ufundishaji. Hatimaye, wakuu wa shule wanahitaji kujiamini katika kufanya maamuzi. Robo ya wakuu wa shule katika nchi zilizo kwenye kiwango cha juu miongoni mwa nchi zenye mapato ya wastani na katika nchi zenye mapato ya juu wameeleza haja ya kupata mafunzo ya masuala haya. Maarifa maalum yanahitajika ili kutekeleza sera za ujumuifu na mageuzi dijitali. Masuala mengine ya sera za elimu, kama vile utunzaji wa mazingira, afya na lishe, pia yatahitaji viongozi wa shule wakuze uwezo wao.

Huku majukumu ya uongozi yakiongezeka, mara nyingi wajibu huu unahusishwa na msongo na uchovu kupita kiasi. Hivyo basi ni muhimu kuhakikisha kwamba huduma za kitaalamu za ushauri na za afya ya akili zinapatikana na kukuza mtandao wa usaidizi katika mazingira ya shule ambapo viongozi wanaweza kujadili changamoto na kupata usaidizi. Gharama ya uwekezaji huu zitasawazika kwa sababu viongozi wa shule wanaopata usaidizi bora wana uwezekano mdogo wa kuacha kazi.

***c. Weka na utekeleze viwango vya uongozi wa shule na upongeze utimizaji wake***

Duniani, karibu nusu ya nchi zimepitisha viwango huru vya kitaaluma vya kitaifa au mifumo ya ustadi inayobainisha ujuzi unaohitajika kwa wakuu wa shule waliopo na wanaoazimia wadifha huu na kueleza utendaji unaofaa. Viwango ni muhimu hasa ambapo wakuu wa shule wanadhaniwa kutekeleza wajibu wa utawala na usimamizi tu. Viwango vinasaidia kuwasilisha vipaumbele vya kitaifa na vinaweza kutumiwa kuelekeza uajiri, matayarisho na mafunzo. Lakini havistahili kuondoa uanuai na vinafaa kudhihirisha muktadha wa kielimu na kitamaduni wa nchi, huku vikiepuka mvuto wa kuiga viwango vya nchi zingine bila kuvirekebisha kulingana na muktadha wa eneo.

Utendakazi wa viongozi wa shule unafaa kutathminiwa kulingana na viwango hivi na matokeo ya elimu yanayonuiwa. Kusudi la msingi la tathmini hizo linafaa kuwa kujenga: kutoa maarifa na kupendekeza mabadiliko katika utendaji. Mifumo ya tathmini inaweza kutumiwa kama msingi wa kubuni mchakato wa uthibitishaji wa kuhitimu unaotambua stadi za kitaaluma za viongozi wa shule. Mifumo ya tathmini iliyoratibiwa vyema inaweza pia kutumiwa kubuni hatua za kuendelea kikazi.

## PENDEKEZO LA 3. SHIRIKI

### *Kuza uongozi wa pamoja na utamaduni wa ushirikiano katika shule*

Wakati mwingine uongozi huonekana kama mfululizo wa vitendo vya kishujaa. Lakini viongozi wa shule si mashujaa na hawastahili kuonekana kama mashujaa; hawawezi kufanya kila kitu na kukifanya peke yao. Wanahitaji kuongoza kwa ushirikiano ili kutimiza malengo ya pamoja, ili wadau wote wawe na motisha ya kufanya kazi kuelekea lengo moja, kila mmoja akitumia uwezo wake maalum.

Hadhi ya uongozi inahitaji kuwa na msingi imara kuliko wadhifa wenye mamlaka. Inahitaji kugharamiwa kupitia vitendo vya kila siku vinavyodhihirisha uadilifu, kujitolea, ujuzi na utu. Sifa hizi huimarisha wakati majukumu ya uongozi yanashirikiwa, kwa njia rasmi au isiyo rasmi, kwa washiriki wa timu ya usimamizi (k.m naibu mkuu wa shule au wakuu wa idara), walimu na wafanyakazi wasaidizi wa shule, wanafunzi, wazazi na wanajamii. Wakuu wa shule wanahitaji kufahamu jinsi ya kutumia kwa ufanisi mifumo, kama vile kamati za usimamizi wa shule na mabaraza ya wanafunzi, kama majukwaa ya mashauriano na ushirikiano. Mahusiano kama hayo ya ushirikiano humairisha uongozi, huboresha michakato ya kufanya maamuzi, huendeleza uwajibikaji na kukuza mazingira jumuifu na nyumbufu. Sera za uongozi wa pamoja shuleni zinafaa kubuniwa na kutekelezwa. Lakini ni nusu tu ya nchi zinasisitiza ushirikiano na walimu katika viwango vyao vya uongozi. Na ni kama theluthi ya mipango ya mafunzo ya uongozi iliyochambuliwa kwa ajili ya ripoti hii inazingatia suala la kuwatayarisha viongozi wa shule kugawa majukumu kwa uwazi, ushirikiano na ubia.

Kwa hivyo, mipango ya maendeleo ya kitaaluma inastahili kuwasaidia wakuu wa shule kubainisha wajibu, kugawa majukumu, kuwawesha wafanyakazi wenza, wanafunzi na wazazi na kutambua michango yao ya kipekee, kukuza mazingira ambapo kila mtu anahisi kwamba anathaminiwa, kuweka njia wazi za mawasiliano na mbinu za kupata maoni mara kwa mara, kukuza timu na kuona shule kama asasi ya mafunzo inayofanya kazi kuelekea malengo ya pamoja.

## PENDEKEZO LA 4. WEKEZA KATIKA VIONGOZI WA MIFUMO

### *Kuza uwezo wa maafisa wa elimu kuwa viongozi wa mifumo*

Viongozi wa mifumo ya elimu ni miongoni mwa wahusika wa elimu ambao hawajatafitiwa sana – na inawezekana kwamba pia hawatayarishwi vya kutosha. Ilhali wanakabidhiwa majukumu makubwa ya kuanzisha na kutekeleza mageuzi ya mifumo ya elimu yanayohimizwa na serikali na kuimarisha michakato ya kuhakikisha ubora. Wakati mwingine, badala ya kuwezeshwa, majukumu yao hupewa wakandarasi au kuhamishiwa kwenye mifumo mipya ya utawala.

Changamoto zile zile zinazoathiri utaalamishaji wa kazi ya wakuu wa shule zinajitokeza hata zaidi kwa wafayakazi hawa wa serikali. Michakato ya ajira na uteuzi hubadilika polepole kwa sababu mageuzi ya utawala wa umma hufanyika polepole. Matayarisho na maendeleo ya kitaaluma hukwama kwa sababu huenda ujuzi wa sekta ya elimu si sharti. Hali hii huifanya vigumu sana kwa maafisa kutekeleza mojawapo ya majukumu yao makuu: kuongoza usaidizi wa ufundishaji. Wao pia huona kazi yao kama ya udhibiti badala ya usaidizi. Mbinu za tathmini za kazi hazina malengo yanayopimika, ambayo yangetumika kutoa mwitiko.

Mipango ya maendeleo ya kitaaluma inahitaji kukuza uwezo wa maafisa wa elimu, huku ikisisitiza sana uongozi elekezi na uhakikishaji wa ubora. Katika mazingira yanayozidi kuwa changamano, maafisa wa elimu pia wanahitaji matayarisho ya udhibiti wa matatizo.

# Kufuatilia elimu katika Malengo ya Maendeleo Endelevu

## UJUMBE MUHIMU

**Hivi leo, watoto wengi zaidi wako shuleni na wanaendelea na elimu kuliko wakati mwingine wowote hapo awali.**

- Kiwango cha watoto walio chini ya umri wa miaka mitatu kushiriki katika elimu kimeongezeka ulimwenguni kote na hasa, kwa zaidi ya asilimia 10 katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara katika kipindi cha miaka kumi iliyopita.
- Tangu mwaka wa 2015, watoto, mabarobaro na vijana milioni 110 zaidi wameingia shule.
- Viwango vya kumaliza shule pia vinaongezeka: Hivi leo, vijana milioni 40 zaidi wanamaliza elimu ya sekondari ikilinganishwa na mwaka wa 2015.
- Tangu mwaka wa 2010, uwiano wa jumla wa usajili katika elimu ya juu kilikuwa kuanzia asilimia 30 hadi takriban asilimia 43, na haraka zaidi katika Amerika ya Kilatini na Karibi na katika Asia ya Mashariki na Kusini Mashariki.

**Lakini ni vigumu zaidi kuwafikia walioachwa nyuma, hali inayokwamisha au, katika hali za mizozo, kurudisha nyuma maendeleo ya elimu.**

- Kiwango cha wanaojiunga shuleni katika umri wa miaka tano kimekwamia takriban asilimia 75 katika mwongo uliopita.
- Duniani, watoto na vijana milioni 251 wangali hawako shuleni, idadi ambayo imepungua kwa asilimia moja tu tangu mwaka wa 2015. Kati ya hawa, milioni 129 ni wavulana na milioni 122 ni wasichana. Hali ya kutengwa inazidishwa na kaida za kijamii na umaskini. Nchini Afghanistan na Niger, watoto, mabarobaro na vijana sita hivi kati ya kila kumi hawako shuleni.
- Watoto wengi mno Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara huanza shule wakiwa wamechelewa na kurudia madarasa. Asilimia 26 wamezidi umri unaofaa wa darasa lao kwa angalau miaka miwili; asilimia 35 wamezidi umri unaofaa katika sekondari za ngazi ya chini.
- Kiwango cha kumaliza elimu ya sekondari kiliongezeka kutoka asilimia 53 mwaka 2015 hadi asilimia 59 katika mwaka wa 2023. Duniani, wanafunzi milioni 650 hutoka shule bila kupata cheti cha elimu ya sekondari.
- Mapengo ya kijinsia katika viwango vya kukamilisha elimu ya sekondari yamezibwa duniani kote, lakini yangali makubwa Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara na maendeleo ya kuyaziba katika mwongo uliopita yamekuwa nusu ya yale ya Asia ya Kati na ya Kusini; eneo lingine ambapo viwango vya wasichana viko chini ya vya wavulana.
- Asilimia ya watu wazima ambao angalau wamekamilisha elimu ya sekondari imeongezeka kwa wastani wa pointi tano za asilimia katika miaka kumi iliyopita. Kwa kasi hii, itachukua miaka mingine 80 kufikia ukamilishaji wa elimu ya sekondari kwa wote.
- Ni asilimia tatu ya watu wazima hushiriki katika elimu na mafunzo. Viwango vya kushiriki vimepungua katika zaidi ya nusu ya nchi zenye data ya mienendo kuanzia mwaka wa 2015.
- Kulikuwa na jumla ya mashambulizi 3,000 ya shule katika mwaka wa 2022, hali iliyofanywa mbaya zaidi na vita nchini Ukreini, na tena katika mwaka wa 2023 na vita katika Mamlaka ya Palestina. Kufikia Julai 2024, asilimia 61 ya shule huko Gaza zilikuwa zimeshambuliwa moja kwa moja.

**Viwango vinavyowekewa walimu mara nyingi huwa vya chini sana au havitimizwi.**

- Ukosefu wa walimu wa kutosha darasani unaweza kutokana na uhaba wa wanaoomba kazi au uhaba wa nafasi za kazi. La kwanza linajitokeza zaidi katika nchi zilizostawi: ni asilimia 4 tu ya vijana wa miaka 15 katika nchi tajiri wangependa kuwa walimu. La pili linajitokeza zaidi katika nchi naskini: nchini Senegal, kulikuwa na ziada ya walimu 1,000 waliohitimu katika mwaka wa 2020 pekee.
- Walimu wengi hawana kiwango cha chini cha kuhitimu kinachohitajika. Katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, kiwango kilipungua kutoka asilimia 70 katika mwaka wa 2012 hadi asilimia 64 katika mwaka wa 2022. Huko Ulaya na Amerika Kaskazini, kiwango kilipungua kutoka asilimia 98 katika mwaka wa 2010 hadi asilimia 93 katika mwaka wa 2023.
- Viwango vinatofautiana katika maeneo mbalimbali. Nchi

nyingi zinahitaji walimu wawe na shahada ya kwanza kufunza katika shule za msingi, ilhali katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, asilimia 17 ya nchi zinakubali cheti cha sekondari ya ngazi ya chini.

**Viwango vya matokeo ya elimu vilikuwa vinapungua hata kabla ya COVID-19, lakini janga hilo linasadifiana na kuchapuka kwa mtindo huo.**

- Ni vigumu kubainisha mienendo, kwa sababu kuna pengo kubwa katika uwakilishi wa data duniani kote: uwakilishi wa chini katika data kuhusu tathmini za elimu unamaanisha kwamba hakuna taarifa kuhusu watoto milioni 680.
- Ushahidi kutoka nchi 70 zilizo kwenye kiwango cha juu miongoni mwa nchi zenye mapato ya wastani na zenye mapato ya juu zilizoshiriki katika utafiti wa PISA wa 2022 (mwishoni wa elimu ya sekondari ya ngazi ya chini) unaonyesha kwamba sehemu ya wanafunzi wenye umilisi wa kusoma ilipungua kwa pointi 9 za asilimia kati ya 2012 na 2018, na kwa pointi nyingine 3 kufikia asilimia 47 katika mwaka wa 2022.
- Sehemu ya wanafunzi wenye umilisi wa hisabati iliongezeka kwa pointi 2 za asilimia kati ya 2012 na 2018, lakini ikapungua kwa pointi 8 kufikia asilimia 36 katika mwaka wa 2022. Huenda kulikuwa na kupungua kwa muda mrefu kuanzia mwaka wa 2009. Janga la COVID-19 lilichapuza kupungua huku lakini linaweza kuficha masuala mengine ya kimfumo.
- Ushahidi kutoka nchi 6 za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ambazo zilishiriki katika tafita za AMPL za 2021 na 2023 (mwishoni wa elimu ya msingi) unaonyesha kwamba ni mwanafunzi mmoja tu kati ya kila kumi walifikia umilisi wa chini kabisa wa kusoma, na wawili kati ya kila kumi katika hisabati.

**Teknolojia inasaidia wanafunzi ambao hawangeweza kupata elimu kuipata, lakini inaleta matatizo mapya.**

- Katika elimu ya sekondari za ngazi za juu, shule nane kati ya kila kumi zimeunganishwa kwenye intaneti. Hatua zilizopigwa na nchi kuelekea vigezo vya muunganisho zimekosa shabaha kwa pointi tatu za asilimia tu.
- Kuna tofauti kubwa kati ya nchi mbalimbali katika ufahamu wa shughuli za msingi za kompyuta: Watu nane kati ya kila kumi katika nchi zenye mapato ya juu, lakini watatu tu kati ya kila kumi katika nchi zenye mapato ya wastani, wanaweza kutuma barua pepe yenye kiambatisho.
- Kuhusiana na shughuli za simu mahiri, asilimia 51 ya vijana na watu wazima walikuwa na uwezo wa kuweka vipengele vya usalama wa vifaa dijitali ikilinganishwa na asilimia 9 katika nchi zenye mapato ya wastani.
- Elimu rasmi inahusishwa na kiwango cha juu cha upataji wa ujuzi dijitali. Katika Umoja wa Ulaya, sehemu ya watu wazima wenye ujuzi dijitali wa msingi inaongezeka kutoka asilimia 34 miongoni mwa wale wenye elimu ya sekondari ya ngazi ya chini hadi asilimia 51 kwa wale walio na elimu ya sekondari ya ngazi ya juu, na asilimia 80 kwa wale walio na elimu ya baada ya sekondari.
- Ongezeko la kasi zaidi la kiwango cha uonevu dhidi ya wasichana ikilinganishwa na wavulana linaendana na hali yao kuwa katika hatari zaidi ya uonevu wa mtandaoni. Wasichana wapo katika hatari zaidi, kwa kiasi fulani ikiwa kwa sababu wanatumia muda zaidi kwenye mitandao jamii.

**Mabadiliko ya tabianchi yanaleta changamoto kwa miundomsingi na mitalaa.**

- Duniani, karibu moja kati ya kila shule nne za msingi hazina huduma msingi za maji ya kunywa, usafi na udhibiti wa afya, ilhali serikali bado zinahitaji kuwekeza zaidi kulinda wanafunzi na shule dhidi ya ongezeko la halijoto na maafa asilia.
- Kiashiria kipya kinachofuatilia maudhui ya elimu ya uendelevu kinaonyesha kwamba masuala ya mabadiliko ya tabianchi yanahitaji kufunzwa zaidi katika madarasa ya awali na katika masomo mbalimbali wala si somo la sayansi tu.

**Uwekezaji katika elimu unapungua katika ngazi za kitaifa na kimataifa.**

- Duniani, matumizi ya serikali katika elimu yalipungua kwa pointi 0.4 za asilimia ya Pato la Taifa kati ya 2015 na 2022: kiwango cha kati kilipungua kutoka asilimia 4.4 hadi asilimia 4.
- Sehemu ya elimu katika jumla ya matumizi ya serikali ilipungua kwa pointi 0.6 za asilimia kutoka asilimia 13.2 katika mwaka wa 2015 hadi asilimia 12.6 katika mwaka wa 2022.
- Mzigo unaozidi kuwa mzito wa kulipa madeni unaathiri matumizi ya fedha katika elimu. Nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara zilitumia karibu kiasi sawa cha fedha kulipia madeni kama zilivyotumia katika elimu katika mwaka wa 2022.
- Kuhusiana na vigezo pacha vya kimataifa vya kutumia angalau asilimia 4 ya Pato la Taifa na angalau asilimia 15 ya matumizi ya serikali katika elimu, nchi 59 kati ya 171 hazikutimiza kigezo chochote kati ya hivyo viwili.
- Matumizi ya fedha kwa kila mtoto hayajabadilika vile tangu mwaka wa 2010.
- Sehemu ya ufadhili unaoelekezwa kwa elimu ilipungua kutoka asilimia 9.3 katika mwaka wa 2019 hadi asilimia 7.6 katika mwaka wa 2022.

## UTANGULIZI

**Kongamano la kwanza La Data na Takwimu za Elimu** (EDS Conference) lilipangwa na Taasisi ya Takwimu ya UNESCO mnamo Februari 2024 jijini Paris, kwa ushirikano na timu ya Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu. Wawakilishi kutoka zaidi ya nchi 130 walihudhuria. Kongamano hili lina malengo matatu makuu: kujenga jumuiya ya kimataifa ya wataalamu wa takwimu za elimu wanaoongoza Kikundi cha Ushirikiano wa Kiufundi (TCG) kuhusu viashiria vya SDG 4; kuwasilisha, kujadili na kufikia makubaliano juu ya dhana, ufafanuzi, mbinu na masuala ya michakato ya tathmini za viashiria katika mfumo wa mapendekezo na miongozo ya kupitishwa kama viwango vya kimataifa; na kujadili athari za maendeleo ya kiteknolojia kwenye takwimu za elimu. Lilikuwa kongamano la kwanza katika msururu; litafanyika kila baada ya miaka mitatu na maamuzi yake yatatekelezwa na Kikundi cha Ushirikiano wa Kiufundi (TCG), ambacho sasa kimebadilishiwa jina na kuitwa Tume ya Data na Takwimu za Elimu. Kongamano la EDS liliziba pengo muhimu. Kwa minajili ya kulinganisha, Kongamano la Kimataifa la Wataalamu wa Takwimu za Kazi, ambalo limekuwa likifaya kazi kusanifisha takwimu za kazi, liliadhimisha karne ya kuwepo katika mwaka wa 2023.

Toleo la pili la **Tathmini ya Maendeleo ya SDG 4** (SDG 4 Scorecard) lilizinduliwa katika Kongamano la EDS. Ni muhtasari wa kila mwaka wa maendeleo ya nchi kuelekea malengo au vigezo vya kitaifa vya 2025 na 2030, mchakato ambao umekita mizizi kufikia sasa. Kufikia sasa, asilimia 77 ya nchi zimewasilisha angalau kigezo kimoja, na asilimia 7 nyingine ya nchi, ambazo ni wanachama wa Jumuiya ya Karibi na Umoja wa Ulaya, zimeafiki malengo yao ya kikanda.


Kwa jumla, nchi zimeweka asilimia 54 ya takwimu zote za malengo ya mwaka wa 2025 hadi 2030. Viashiria ambavyo vimeteuliwa zaidi kama vigezo ni kiwango cha ushiriki katika elimu ya awali ya utotoni (asilimia 72) na kiwango cha kukamilisha elimu ya sekondari (asilimia 70). Viashiria ambavyo havijateuliwa sana ni pengo la kijinsia katika ukamilishaji wa elimu ya sekondari (asilimia 36) na kigezo kipya cha muunganisho wa intaneti katika shule (asilimia 33).

Wakati Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa lilipitisha mfumo wa kimataifa wa viashiria vya malengo ya maendeleo endelevu (SDG) mnamo 2017, iliratibu michakato miwili ya Tathmni za Kina ambayo ingeongozwa na Kikundi cha Wataalamu cha Mashirika ya Kimataifa kuhusu Viashiria vya SDG. Mchakato wa kwanza (2019-2020), ambapo kiwango cha kukamilisha kilipitishwa kama kiashiria cha kimataifa, ulizingatia mbinu za kutathmini viashiria. Wa pili unafanyika kati ya mwaka wa 2024 na 2025 na unazingatia uwakilishi wa data kuhusu viashiria: data ya angalau asilimia 40 ya nchi na ya watu lazima iwepo, angalau katika maeneo ambapo kiashiria husika ni muhimu. Kigezo hiki kinaathiri viashiria kadhaa vya SDG 4, hasa: asilimia ya watoto ambao wanaendelea kukua vyema (4.2.1), umilisi wa kiutendaji wa kusoma, kuandika na hisabati (4.6.1) na umilisi wa chini kabisa wa kusoma na hisabati (4.1.1). Kigezo hicho cha mwisho kina data wakilishi vya kutosha mwishoni mwa elimu ya msingi (b) na ya sekondari za ngazi ya chini (c), lakini data inapatikana kwa ajili ya asilimia 16 ya watu na asilimia 20 ya nchi katika kiwango cha darasa la 2/3 (a). Juhudi zinaendelea kuhakikisha kwamba nchi nyingi zaidi zinakusanya data kama hiyo, lakini pia ziripoti data kuhusu baadhi ya stadi za awali, ijapokuwa kwa sasa nchi hizo hazitimizi vigezo vya kuripoti kuhusu kiwango cha umilisi wa chini kabisa, ili kuwezesha baadhi ya tathmini kufanywa.

## LENGO LA 4.1. ELIMU YA MSINGI NA YA UPILI

Inakadiriwa kwamba watoto na vijana milioni 251 hawakuwa shuleni katika mwaka wa 2023. Ijapokuwa kama watoto, mabarobaro na vijana milioni 110 zaidi wameingia shuleni tangu mwaka wa 2015, idadi ya wasio

**MCHORO WA 5:**
**Tangu 2015, idadi ya wasio shuleni haijabadilika sana**
*Kiwango cha wasio shuleni, watoto wasio shuleni na watoto waliosajiliwa katika elimu ya msingi na ya sekondari, 2000-2023*




*GEM StatLink:* https://bit.ly/GEM2024_Summary_fig5
*Chanzo:* Hifadhidata ya VIEW.

shuleni imepungua kwa milioni tatu tu, au asilimia moja, kwa wakati huo (**Mchoro wa 5**). Kinyume na hilo, katika miaka nane kabla ya mwaka wa 2015, idadi ya wasio shuleni ilikuwa imepungua kwa milioni 43, yaani kwa asilimia 14. Kwa hivyo kasi ya maendeleo imepungua kwa zaidi ya asilimia 90. Kadirio hili halijumuishi baadhi ya vikundi vilivyoathiriwa na mizozo, ambapo michakato ya ukusanyaji data imevurugwa. Kwa mujibu wa kadirio moja, kujumlisha idadi inayokisiwa ya watoto wasio shuleni katika nchi tano zenye dharura kubwa zaidi – Burkina Faso, Myanmar, the Mamlaka ya Palestina, Sudan Kusini na Sudan – kungeongeza idadi ya wasio shuleni kwa milioni 5.5


Kiwango cha wasio shuleni kilipungua kutoka asilimia 17.2 katika mwaka wa 2015 hadi asilimia 16.1 katika mwaka wa 2023. Miongoni mwa watoto wa umri wa kwenda shule, mabarobaro na vijana, kiwango kilikuwa asilimia 33 katika nchi zenye mapato ya chini, asilimia 19 katika nchi zilizo kwenye kiwango cha chini miongoni mwa nchi zenye mapato ya wastani, asilimia 8 katika nchi zilizo kwenye kiwango cha juu miongoni mwa nchi zenye mapato ya wastani, na asilimia 3 katika nchi zenye mapato ya juu. Duniani, kama asilimia 10 ya watoto wa umri wa shule ya msingi, asilimia 14 ya mabarobaro wa umri wa sekondari ya ngazi ya chini na asilimia 30 ya vijana wa umri wa sekondari ya ngazi ya juu hawako shuleni. Hali ya kutobadilika ilianza katika mwaka wa 2015 au kidogo kabla ya hapo. Hali hii ilikuwepo kabla ya janga la COVID-19 na haionekani kuhusiana nalo.

Viwango vya ukamilishaji vimeongezeka ijapokuwa polepole. Kiwango cha kumaliza elimu ya msingi kiliongezeka kutoka asilimia 85 hadi asilimia 88, yaani kwa pointi 3.1 za asilimia kati ya 2015 na 2023, na kiwango cha kumaliza elimu ya sekondari za ngazi ya chini kiliongezeka kutoka asilimia 74 hadi asilimia 78, yaani kwa pointi 4 za asilimia. Kiwango cha kumaliza elimu ya sekondari kiliongezeka kutoka asilimia 53 hadi asilimia 59, yaani kwa pointi 5.9 za asilimia, sawa na

**MCHORO WA 6:**

**Tangu mwaka wa 2012, asilimia ya wanaofikia umilisi wa chini kabisa umepengua kwa pointi 12 za asilimia kwa kusoma na pointi 6 za asilimia katika hisabati**

*Asilimia ya wanafunzi waliofikia umilisi wa chini kabisa mwishoni mwa elimu ya sekondari za ngazi ya chini, nchi zilizochaguliwa zenye mapato ya wastani na ya juu, 2012, 2018 na 2022*




*GEM StatLink:* https://bit.ly/GEM2024_Summary_fig6
*Chanzo*: Uchambuzi wa timu ya Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu kutokana na data ya PISA.

ongezeko la pointi 0.7 za asilimia kila mwaka. Kuwajumuisha wanaokamilisha kila awamu wakiwa wamechelewa kuongeongeza kiwango cha kukamilisha kwa pointi 4.4. za asilimia katika elimu ua msingi na ya sekondari za ngazi ya chini na kwa pointi 3.3 za asilimia katika elimu ya sekondari za ngazi ya juu. Hii inamaanisha kwamba, kwa mfano, hatimaye asilimia 62 ya vijana humaliza elimu ya sekondari ya ngazi ya juu. Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara ndilo eneo lenye tofauti kubwa zaidi kati ya viwango vya kumaliza kwa wakati na kumaliza hatimaye. Katika mwaka wa 2023, asilimia 67 ya watoto walikuwa wamemaliza elimu ya shule ya msingi kwa wakati, lakini asilimia 78 walimaliza wakiwa wamechelewa kwa miaka kadhaa, tofauti ya pointi 10.4 za asilimia

Duniani, inakadiriwa kwamba mwishoni mwa elimu ya shule ya msingi, asilimia 58 ya wanafunzi hufikia umilisi wa chini kabisa wa kusoma, na asilimia 44 wa hisabati. Vivyyo hivyo, mwishoni mwa elimu ya sekondari za ngazi ya chini, asilimia 64 ya wanafunzi hufikia umilisi wa chini kabisa wa kusoma, na asilimia 51 wa hisabati. Suala la athari ambazo huenda zilitokana na janga la COVID-19 kwenye matokeo ya mafunzo limezingatiwa sana kwa sababu ya kukatizwa kwa masomo shule zilipofungwa. Kuzinduliwa kwa ripoti ya PISA ya 2022, ambayo hutathmini wanafunzi mwishoni wa elimu ya sekondari za ngazi ya chini, kunatoa nafasi ya kushughulikia suala hili. Kwa upande wa kusoma, sehemu ya wanafunzi waliofikia umilisi wa chini kabisa ilipungua kwa pointi tisa za asilimia kutoka mwaka wa 2012 hadi 2018 na tena kwa pointi zingine tatu katika mwaka wa 2022 (**Mchoro wa 6a**). Kwa upande wa kusoma, sehemu ya wanafunzi waliofikia umilisi wa chini kabisa ilipungua kwa pointi tisa za asilimia kutoka mwaka wa 2012 hadi 2018 na tena kwa pointi zingine tatu katika mwaka wa 2022 (**Mchoro wa 6b**).

## LENGO LA 4.2. KIPINDI CHA AWALI CHA UTOTONI

Katika mwongo uliopita, kiwango cha kushiriki katika elimu ya kipindi cha awali cha utotoni kimeongezeka kwa watoto wachanga (wenye mika sifuri hadi mitatu) lakini hakijabadilika vile kwa watoto wenye umri unaozidi huo. Kati ya 2013 na 2023, sehemu ya watoto walioingia shule mwaka mmoja kabla ya umri rasmi wa kuingia shule ya msingi imebaki asilimia 75 hivi, ijapokuwa iliongezeka kwa kama pointi saba za asilimia Afrika Kaskazini na Asia Magharibi (kufikia asilimia 51) na Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara (kufikia asilimia 49), maeneo mawili yaliyobaki nyuma zaidi katika hili.

Kuanza elimu ya msingi mapema kunatatiza uchambuzi wa kiashiria cha kimataifa cha SDG 4.2.2, ambacho hakitofautishi kati ya wale walio katika elimu ya chekechea na wanaoingia shule ya msingi mwaka mmoja mapema. Katika angalau nchi 49, zaidi ya asilimia tano ya watoto wamesajiliwa katika elimu ya msingi mwaka mmoja kabla ya umri rasmi wa kuingia kiwango hicho (**Mchoro wa 7**). Kuondoa watoto waliosajiliwa katika elimu ya msingi kungesababisha punguo la asilimia 20 katika kiashiria hicho. Nchini Burundi, ambapo umri wa kuingia shule ya msingi ni miaka saba, karibu asilimia 90 ya watoto wa umri wa miaka sita wamesajiliwa katika elimu ya msingi badala ya elimu ya chekechea. Nchini Burkina Faso, usajili halisi wa watoto mwaka mmoja kabla ya umri rasmi wa kuingia shule ya msingi umeongezeka pakubwa kutoka asilimia tatu 2011 hadi asilimia 21 katika mwaka wa 2020. Hata hivyo, sehemu kubwa ya ongezeko hili ilitokana na ongezeko la usajili wa mapema katika elimu ya msingi

Kuhudhuria elimu ya chekechea inahusishwa na maendeleo bora zaidi ya watoto kwa kijumla. Matokeo kutoka kwa nyenzo mpya ya ufuatiliaji ya UNICEF, Kielezo cha Maendeleo ya Kipindi cha Awali cha Utotoni 2030, kinaonyesha kwamba watoto ambao ni tajiri zaidi na wale wanaohudhuria shule za chekekechea wana uwezekano mkubwa zaidi wa kuwa wanaendelea kukua vizuri. Nchini Eswatini, asilimia 74 ya watoto wanaohudhuria elimu ya chekechea wanaendelea kukua vizuri, ikilinganishwa na asilimia 38 kwa wale ambao hawadhurii. Mazingira ya kuwezesha nyumbani yanaweza kuimarisha ukuaji wa watoto, ikiwa ni pamoja na utayari wa kwenda shule, ujuzi wa mapema wa kusoma, kuandika na hisabati, na ujuzi wa kijamii na kihisia. Hata hivyo, katika angalau nchi kumi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara, zaidi ya asilimia 30 ya watoto waliachwa bila uangilizi wa kutosha. Isitoshe, walezi wa watoto wanahitaji mafunzo. Utafiti wa walezi wa watoto katika nchi zenye mapato ya chini na ya wastani ulipata kwamba ni nusu yao tu walishiriki katika shughuli muhimu za kuchochea ujifunzaji na utayari wa kwenda shule.

Uongozi wa elimu ya chekechea ni muhimu, hasa uongozi wa ufundishaji, ingawa viongozi wengi wa chekechea hawapati matayarisho wala hawana vigezo vya kujitahidi kutimiza. Majukumu mengi huwa ya usimamizi. Nchini Israel na Uturuki, viongozi wa elimu na utunzaji wa watoto wachanga (ECCE) hutumia chini ya asilimia 20 ya muda wao katika uongozi wa ufundishaji.


## LENGO LA 4.3. ELIMU YA KIUFUNDI, YA KITAALAMU, ELIMU YA JUU NA YA WATU WAZIMA

Kiwango cha kati cha watu wazima kushiriki katika elimu na mafunzo rasmi na yasiyo rasmi ni asilimia 3. Kiwango hiki kinazidi asilimia 5 katika nch 40 na kinazidi asilimia 10 katika nchi 15, nyingi ambazo ni zenye mapato ya juu. Katika nchi 78 zilizokuwa na data, kati ya mwaka wa 2013 na 2023,

**MCHORO WA 7:**

**Watoto wengi wamesajiliwa katika elimu ya msingi mwaka mmoja kabla ya umri rasmi wa kuingia kiwango hicho**

Sehemu ya watoto ambao wamesajiliwa katika elimu ya msingi mwaka mmoja kabla ya umri rasmi, kulingana na kiwango cha elimu, 2018–2020




*Zingatia*: Katika nchi zilizoonyeshwa, angalau asilimia tano ya watoto wamesajiliwa katika elimu ya msingi mwaka mmoja kabla ya umri rasmi wa kuingia kiwango hicho.

*GEM StatLink:* https://bit.ly/GEM2024_Summary_fig7

*Chanzo*: Hifadhidata ya UIS.

kiwango cha kati cha watu wazima kushiriki kilipungua kwa pointi 0.5 za asilimia. Hii inaashiria kwamba data ya nchi zenye mapato ya juu, ambazo zina kiwango cha juu cha kushiriki na kiwango cha juu cha kuripoti, inarejelea mwaka wa 2022 na nchi hizi bado zilikuwa zinakabiliana na athari za COVID-19. Katika suala la tofauti kati ya jinsia, hali katika nchi zilizostawi inatofautiana sana na hali katika nchi maskini. Katika nchi zenye mapato ya juu, wanaume 73 wanashiriki katika elimu na mafunzo kwa kila wanawake 100, ilhali katika nchi zenye mapato ya chini, ni wanawake 50 tu wanaoshiriki kwa kila wanaume 100.

Kiwango cha kati cha usajili katika elimu na mafunzo ya kiufundi na kitaalamu (TVET) iliongezeka kutoka asilimia 2 hadi asilimia 5 kati ya mwaka wa 2010 na 2023. Katika nchi 38 ambazo zina data, kulikuwa na takriban wanawake

80 waliosajiliwa katika TVET kwa kila wanaume 100, huku hali ikiwa kinyume cha hiyo katika elimu ya juu. Katika nchi nane, wanaume walikuwa na uwezekano mkubwa zaidi wa kushiriki katika elimu ya juu na ya TVET, na katika nchi sita, idadi ya wanawake ilizidi ile ya wanaume katika zote mbili. Uwiano wa jumla wa usajili katika elimu ya juu uliongezeka kutoka asilimia 30 katika mwaka wa 2010 hadi asilimia 37 katika mwaka wa 2015, na asilimia 43 katika mwaka wa 2023. Uwiano katika usajili uliongezeka kwa kasi katika kipindi hiki katika Amerika ya Kilatini na Karibi (kwa pointi 16 za asilimia) na katika Asia ya Mashariki na ya Kusini Mashariki (kwa pointi 34 za asilimia). Tofauti na hilo, uwiano ulipungua barani Oshenia na kutobadilika katika Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Viongozi wa elimu ya juu wanakabiliwa na changamoto kubwa kama vile mabadiliko ya kasi ya teknolojia, mizozo ya kisiasa, matakwa ya pesa za umma, utofauti zaidi wa wanafunzi na uchunguzi zaidi. Ilhali, mara nyingi hawana uhuru wa kufanya maamuzi. Karibu asilimia 40 ya nchi hazitambui uhuru wa taasisi kisheria. Viongozi wengi ni wasomi waliopandishwa cheo huku wakiwa hawana mafunzo ya usimamizi au wakiwa na mafunzo kidogo, ijapokuwa nchi kadhaa zinashughulikia suala hili kwa kutoa mafunzo. Wanawake hawajawakilishwa ipasavyo katika uongozi wa elimu ya juu, huku wakijumuisha asilimia 25 tu ya viongozi katika vyuo vikuu 200 bora zaidi duniani.

## LENGO LA 4.4. STADI ZA KAZI

Duniani, kuna tofauti katika ukusanyaji wa data kuhusu ujuzi wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), huku nchi zilizostawi zaidi zikiwakilishwa zaidi. Kati ya walioripoti data hii katika mwaka wa 2021, kuna tofauti katika upati wa ujuzi wa TEHAMA. Kwa mfano, asilimia 80 ya vijana na watu wazima katika nchi za kati miongoni mwa zenye mapato ya juu walikuwa na uwezo wa kutuma barua pepe yenye kiambatisho ikilinganishwa na asilimia 32 katika nchi zenye mapato ya wastani. Shughuli mpya zinafuatiliwa kuhusiana na matumizi ya simu mahiri, ijapokuwa data inapatikana kwa nchi chache zaidi. Miongoni mwa nchi zenye mapato ya juu, asilimia 38 ya vijana na watu wazima walikuwa na uwezo wa kuthibitisha kuaminika kwa taarifa za mtandaoni ikilinganishwa na asilimia 10 katika nchi zenye mapato ya wastani. Elimu rasmi ni muhimu katika upataji wa ujuzi dijitali. Katika Umoja wa Ulaya, sehemu ya watu wazima walio na ujuzi dijitali wa msingi ilianzia asilimia 34 miongoni mwa wale ambao walikuwa wamekamilisha elimu ya sekondari ya ngazi ya chini kama kiwango cha juu zaidi hadi asilimia 51 kwa wale waliokamilisha sekondari ya ngazi ya juu na asilimia 80 miongoni mwa wale waliokuwa wamepata angalau masomo fulani ya baada ya sekondari.

Katika nchi ya wastani, sehemu ya watu ambao walikuwa wamemaliza angalau elimu ya sekondari iliongezeka kwa pointi 0.5 za asilimia kwa kila mwaka kati ua 2012-2013 na 2022-2023. Kwa kasi hii, itachukua miaka 80 kufikia ukamilishaji wa elimu ya sekondari kwa wote. Lakini hakuna tofauti kubwa katika kila kundhi la nchi. Kwa mfano, miongoni mwa nchi ambazo zilianzia chini ya asilimia 20 katika kipindi cha 2012-2013, India iliongeza pointi 18 za asilimia katika miaka 10, huku nchini Guatemala, Niger na Senegal, kiwango ni kama hakikubadilika. Miongoni mwa nchi ambazo zilianzia kati ya asilimia 20 na 40 kati ya 2013-2023, Malta iliongeza pointi 21 na Ureno pointi 16 katika kipindi cha miaka 10, huku katika Jamhuri ya Dominika na Hondurasi, kiwango hakijabadilika. Hii inamaanisha kwamba ijapokuwa kuna mienendo dhahiri ya kiwastani, hakuna nchi yeyote ambayo mwelekeo wake unaweza kutabiriwa.

Ujuzi na tabia za uongozi zinaweza kupatikana kupitia elimu. Mafunzo ya uongozi yamepanuka kutoka kuwa shughuli ya kipekee kwa wanafunzi wachache wa ngumbaru na kuwa ya kina zaidi, huku malengo yake yakipanuka ili kuandaa kizazi kijacho, si kwa ajili ya biashara tu bali pia kwa ajili ya utetezi wa kijamii. Ni muhimu kutambua masuala ya kijamii yanayoathiri ujuzi wa uongozi na kutoa fursa sawa kwa vijana wote kukuza ujuzi huu.

## LENGO LA 4.5. USAWA

Duniana kote, usawa wa jinsia karibu umefikiwa kwa wastani katika viwango vya wasio shuleni tangu mwaka wa 2015. Hata hivyo, wavulani zaidi wangali hawako shuleni ikilinganishwa na wasichana huko Asia ya Mashariki na ya Kusini Mashariki, Ulaya na Amerika Kaskazini na Amerika ya Kilatini na Karibi, ambapo pengo limepanuka kutoka wavulana 107 katika mwaka wa 2015 hadi wavulani 113 kwa kila wasichana 100 wasio shuleni katika mwaka wa 2023.

Usawa wa jinsia pia umedumishwa duniani katika viwango vya kumaliza elimu ya msingi na ya sekondari ya ngazi ya chini tangu mwaka wa 2015, lakini hali imegeuka katika elimu ya sekondari za ngazi ya juu: Vijana 97 wa kike walikuwa wanamaliza kwa kila vijana 100 wa kiume katika mwaka wa 2010, lakini vijana 97 wa kiume walikuwa wanamaliza kwa kile vijana 100 wa kike katika mwaka wa 2020. Kuna maeneo mawili yaliyosalia ambapo tofauti katika kiwango cha kumaliza elimu ya sekondari ni hasi kwa upande wa wasichana, lakini Asia ya Kati na ya Kusini imepiga hatua kuelekea usawa kwa kasi maradufu ya ile ya Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Pengo la mahali pia limepungua: katika mwaka wa 2010, vijana 41 walio mashambani walikuwa wanamaliza elimu ya sekondari ya ngazi ya juu kwa kila vijana 100 walio mijini; kufikia mwaka

wa 2022, uwiano huu ulikuwa umeimarika hadi vijana 67 mashambani kwa kila vijana 100 mijini.

Katika nchi zenye mapato ya juu, watu 88 wa kiume wanafikia umilisi wa chini kabisa wa kusoma kwa kila 100 wa kike, huku katika nchi zenye mapato ya wastani, ni 72 tu wa kiume kwa kila 100 wa kike wanafikia kiwango hicho. Kwa wastani, hakuna tofauti kubwa za kijinsia katika umilisi wa hisabati. Lakini ni wanafunzi 47 tu kutoka tabaka la chini kabisa la kijamii na kiuchumi walifikia umilisi wa chini kabisa katika hisabati kwa kila wanafunzi 100 kutoka tabaka la juu zaidi la kijamii na kiuchumi. Lakini ni wanafunzi 60 tu kutoka tabaka la chini kabisa la kijamii na kiuchumi walifikia umilisi wa chini kabisa katika hisabati kwa kila wanafunzi 100 kutoka tabaka la juu zaidi la kijamii na kiuchumi.

Katika mwaka wa 2015, asilimia ya kati ya watoto waliokuwa wakipokea mafunzo kwa lugha yao ya nyumbani katika madarasa ya awali ilikuwa asilimia 84; asilimia hii ya kati ilipungua kidogo hadi 82 kufikia mwaka wa 2022. Data ya mwisho wa shule ya msingi ni chache zaidi, lakini nchi za Afrika zikiwemo Cameroon, Chad, Congo na Côte d'Ivoire zimeonyesha ongezeko kubwa la sehemu ya wanafunzi wanaopokea mafunzo kwa lugha yao ya nyumbani wakati wa kumaliza shule ya msingi

## LENGO LA 4.6. UWEZO WA KUSOMA NA KUANDIKA WA VIJANA NA WATU WAZIMA

Viwango vya wanaoweza kusoma na kuandika vimekua katika miongo iliyopita huku vizazi vikibadilika. Nchi zenye mapato ya chini na zilizo kwenye kiwango cha chini miongoni mwa nchi zenye mapato ya wastani zimeonyesha tofauti kubwa zaidi katika viwango vya kusoma kati ya vizazi, ikidhihirisha kuongezeka sana kwa viwango vya kushiriki katika elimu. Nchini India, ambapo data ilitoka kwenye tafiti za kaya au wafanyakazi, tofauti katika ya viwango vya kusoma na kuandika kati ya vikundi vya vijana (wenye umri wa miaka 15 hadi 24) na vikundi vya wazee (wenye umri wa miaka 65 au zaidi) ni zaidi ya pointi 45 za asilimia. Nchini Msumbiji, ambapo data ya vikundi vyote vya umri ilitoka kwenye Utafiti wa Bajeti za Kaya, kiwango cha kusoma na kuandika cha watu wazima (asilimia 56) ni karibu maradufu ya kile cha wazee (asilimia 29).

Kadri nchi nyingi zinavyofikia uwezo wa kusoma na kuandika kwa vijana wote, tofauti zenye misingi ya kijinsia, mapato na eneo sanasana hutoweka. Nchini Nepal, wanawake wazee 24 pekee wanaweza kusoma na kuandika kwa kila wanaume wazee 100. Pengo la kijinsia linapungua kufikia 73 kwa kila 100 kwa walio na umri wa miaka 25 hadi 64 na usawa umefikiwa kwa walio na umri wa miaka 15 hadi 24. Hata hivyo, vikundi vilivyo katika hali ngumu ambavyo vina viwango vya chini vya uwezo wa kusoma na kuandika vinapatikana hata katika nchi zenye viwango vya juu vya jumla vya uwezo wa kusoma na kuandika. Kwa mfano, nchini Peru asilimia 95 ya watu wazima wanaweza kusoma na kuandika, lakini ni asilimia 78 tu ya wanawake walio mashambani na asilimia 84 ya wanawake walio katika humusi maskini zaidi wana uwezo huo.

Sera za kukuza uwezo wa kusoma katika familia zinastahili kuwa na mtazamo wa muda mrefu katika kubadilisha tamaduni za ujifunzaji, hasa miongoni mwa familia na jamii zilizo katika hali ngumu, za kina na zenye rasilimali za kutosha ili ziwe endelevu; kujitahidi kukuza ujumuifu na hivyo kuziba mapengo ya kijamii, kijinsia, kikabila na kidijitali; kukuza ubia na ushirikiano kote katika idara, wizara na asasi; na kutumia mtazamo wa kujifunza kwa maisha ili kuwahimiza wanafunzi walio katika hali ngumu washiriki na waendelee kushiriki katika mafunzo ya kusoma na kuandika.

## LENGO LA 4.7. MAENDELEO ENDELEVU NA URAIA WA KIMATAIFA

Timu ya Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu, Mradi wa Ufuatiliaji na Utathmini wa Mawasiliano na Elimu ya Tabianchi (MECCE), na UNESCO wameshirikiana kuchambua kiwango cha maudhui kuhusu uendelevu katika mifumo ya mitalaa ya kitaifa na silabasi za masomo ya sayansi na sayansi jamii. Miongoni mwa nchi 76, asilimia 34 ya nchi hazikujumuisha maudhui kuhusu uendelevu katika silabasi ya sayansi jamii katika darasa la tatu, ikilinganishwa na asilimia 21 katika darasa la sita na asilimia 16 katika darasa la tisa (**Mchoro wa 8**). Haionekani kwamba nchi zilizostawi zaidi na nchi zilizo katika hatari zaidi ya kupatwa na madhara ya mabadiliko ya tabianchi ndizo zinajumuisha maudhui zaidi kuhusu uendelevu.


Asilimia ya shule ambazo zinazota mafunzo ya stadi za maisha kuhusu VVU na masuala ya ngono haijabadilika vile kwa muda. Karibu nchi 80 zinaripoti kuhusu kiashiria hiki. Kati ya hizi, theluthi moja zinaripoti kwamba shule zote katika viwango vyote zinatoa elimu ya stadi za maisha kuhusu VVU na masuala ya ngono, zikiwemo Burundi, Thailand na Uruguay. Katika asilimia 10 ya nchi, zikiwemo Aljeria, Mauritania na Uganda, hakuna shule za kiwango chochote zinazotoa maarifa ya aina hii. Ni katika asilimia tisa tu ya nchi ambako hakuna shule za sekondari zinazotoa mafunzo ya stadi za maisha kuhusu VVU na masuala ya ngono, ikilinganishwa na asilimia 25 kwa shule za msingi.

Mipango ya kuelimisha raia sharti ishughulikie changamoto mbili hasa: kwanza, kupungua kwa kiwango cha kujitokeza kwa wapiga kura (k.m. kutoka asilimia 77 katika miaka ya sitini hadi asilimia 67 baada ya mwaka wa 2010 duniani), na pili, mapengo makubwa zaidi ya kijinsia na ya kijamii na

**MCHORO WA 8:**

**Kuna uwezekano mkubwa zaidi wa silabasi kujumuisha maudhui kuhusu uendelevu katika elimu ya sekondari za ngazi ya chini kuliko ya msingi.**

*Sehemu ya nchi ambazo hazijumuishi maudhui yoyote kuhusu uendelevu, kulingana na aina ya hati, darasa na somo*




*GEM StatLink:* https://bit.ly/GEM2024_Summary_fig8
*Chanzo*: Ripoti ya GEM, mradi wa MECCE na hifadhidata ya UNESCO.

kiuchumi katika azma za kisiasa na nia ya kushiriki. Mara nyingi wasichana hukua wakiwa wameshawishika kwamba uongozi wa kisiasa ni shughuli ya wanaume sanasana. Nchini Marekani, katika jaribio ambapo watoto waliulizwa wachore kiongozi wa kisiasa, uwezekano wa wasichana kuchora mwanamume uliongezeka kulingana na umri, kutoka asilimia 47 miongoni mwa wenye umri wa miaka sita hadi asilimia 75 miongoni mwa wenye umri wa miaka 12, ilhali sehemu ya wavulana waliofanya vivyo hivyo haikubadilika sana kwa kila umri, ikipita asilimia 70 kidogo tu. Tafiti za uhusiano kati ya elimu na ushiriki katika kisiasa kwa jumla hazijatoa kauli bayana. Nje ya mafunzo ya darasani, shughuli za ziada na maadili ya shule yanaweza kuathiri mafunzo ya kiraia na kuelekeza utambulisho (wa kikabila, kisiasa au ana nyingine yeyote ya utambulisho binafsi), kiwango cha kujiamini kutenda na kutimiza malengo.

## LENGO LA 4.A. VISTAWISHI VYA ELIMU NA MAZINGIRA YA KUJIFUNZA

Katika mwaka wa 2023, asilimia 77 ya shule za msingi duniani zilikuwa na maji ya kawaida ya kunwya. Kiwango kilikuwa sawa na hicho kwa huduma za msingi za usafi na udhibiti wa afya. Duniani, hatua zimepigwa polepole, lakini nchi chache zimepiga hatua kubwa tangu mwaka wa 2015. Nchini Rwanda, sehemu ya shule za msingi zenye mahali pa kunawia mikono iliongezeka kutoka asilimia 40 katika mwaka wa 2015 hadi asilimia mia katika mwaka wa 2021.

Katika nchi 34 kati ya 66 zenye data, uonevu uliongezeka kwa angalau pointi mbili za asilimia kwa wasichana kati ya 2018 na 2022. Hali ilikuwa vivyo hivyo kwa wavulana katika nchi 22 pekee. Nchini Uturuki, sehemu ya wasichana wa miaka 15 ambao wamepitia uonevu iliongezeka kwa pointi 18 za asilimia ikilinganishwa na pointi saba za asilimia kwa wavulana.

Nchi kumi za juu kulingana na idadi ya mashambulizi ziliwakilisha asilimia 68 ya mashambulizi yote katika elimu katika mwaka wa 2022 na asilimia 80 katika mwaka wa 2023. Tangu 2013, Afghanistan na Mamlaka ya Palestina zimepitia zaidi ya mashambulizi 100 katika elimu kila moja na kila mwaka isipokuwa mmoja. Katika mwaka wa 2023, Mamlaka ya Palestina ilipitia mashumbulizi 720 katika elimu.

Katika mwaka wa 2022, watoto milioni 418 duniani walikuwa wanapata mlo shuleni, milioni 30 zaidi ya ilivyokuwa mwanzoni mwa mwaka wa 2020, kabla ya janga la COVID-19. Uwakilishi wa data unatofautiana sana, kuanzia chini ya asilimia tano ya watoto wa shule ya msingi nchini Aljeria na Cameroon, hadi karibu asilimia mia katika nchi kadhaa za Ulaya a Amerika ya Kilatini. Makadirio haya mara nyingi hupuuza kwamba wanafunzi wengi husomea shule za kibinafsi. Mpango wa milo shuleni nchini Gambia unashughulikia asilimia 47 ya wanafunzi waliosajiliwa, hata hivyo, ukizingatia kwamba kama theluthi ya watoto wa shule ya msingi wapo katika taasisi za binafsi, uwakilishi wa wanafunzi wa shule za umma ni asilimia 70.

Kukabiliana na ongezeko la halijoto linalowadhuru wanafunzi na kudhoofisha uwezo wao wa kuzingatia jambo imekuwa tatizo kubwa katika nchi nyingi. Masuluhisho ni pamoja na vifaa vya bei ya juu kama vile viyoyozi, au hatua rahisi kama vile kupaka kata za nje rangi nyeupe na kutumia pazia na maturubai ya kufunika madirisha/milango. Nchini Indonesia kupaka mapaa meusi rangi nyeupe kulipunguza halijoto la ndani kwa zaidi ya nyusi 10 Selsiasi. Maafa yanayohusiana na hali ya hewa, kama vile mioto ya misitu, dhoruba, mafuriko, ukame na kupanda kwa kiwango cha maji ya bahari, yanaweza kuharibu mifumo ya elimu. Nchi za Visiwa vya Pasifiki zinajumuisha nchi tano kati ya kumi za juu ambazo zimepata hasara kubwa zaidi za kifedha kutokana na kuharibika au kuangamizwa kwa miundomsingi muhimu, ikiwa ni pamoja na shule, kutokana na maafa.

## LENGO LA 4.B. UFADHILI WA MASOMO

Katika mwaka wa 2022, Dola bilioni 4.6 za Marekani za ufadhili rasmi wa maendeleo (ODA) zilitolewa kama ufadhili wa masomo na gharama za wanafunzi, ongezeko la asilimia 31 ikilinganishwa na mwaka wa 2015. Viwango vya ufadhili wa masomo vilipungua sana kwa asilimia 26 kati ya 2019 na 2021 kutokana na janga la COVID-19, na licha ya kuimarika, bado vilikuwa chini kidogo ya viwango vya 2019 katika mwaka wa 2022.

Duniani, idadi ya wanafunzi wa kimataifa wanaondoka kwenda kusoma imeongezeka mara tatu tangu mwaka wa 2000. Miongoni mwa nchi zilizoangaziwa katika lengo la SDG 4b, idadi ya wanafunzi wa kigeni wanaondoka kwenda kusoma iliongezeka polepole Afrika na Nchi Ndogo za Visiwa Zinazoendelea ikilinganishwa na kiwango cha kote duniani na kwa kasi zaidi katika Nchi Zisizostawi. Ufaransa na Ujerumani ndio wafadhili wakuu wanaoripoti kuhusu ufadhili wa masomo na hasa, gharama za matumizi ya wanafunzi kama ODA. Barani Afrika, Ufaransa inawakilisha karibu theluthi mbili za jumla ya ODA na Ujerumani karibu theluthi ya iliyosalia. Nchi zingine zinazotenga fedha za ODA kwa ajili ya ufadhili wa masomo ni pamoja na Hungaria (ambayo ilitumia Dola milioni 31 za Marekani kwa ajili ya wanafunzi kutoka Afrika), Jamhuri ya Korea (ambayo ilitumia Dola milioni 22.5 za Marekani kwa ajili ya wanafunzi kutoka Nchi Zisizostawi), na Australia na New Zealand (ambazo zilitumia Dola milioni 23.5 za Marekani kwa ajili ya wanafunzi kutoka Nchi Ndogo za Visiwa Zinazoendelea).

Sehemu ya ODA ya ufadhili wa masomo kutoka nchi zisizo wanachama wa Kamati ya Ufadhili wa Maendeleo ya OECD iliongezeka kutoka asilimia moja katika mwaka wa 2014 hadi asilimia tisa katika mwaka wa 2022. Katari, Romania, Saudia na Uturuki zimeongeza pakubwa ODA yao ya ufadhili wa masomo, kutoka Dola milioni 29 tu za Marekani katika mwaka wa 2013 hadi Dola milioni 450 za Marekani katika mwaka wa 2022. Tangu mwaka wa 2018, sehemu kubwa ya ODA imeendea wanafunzi kutoka Syria. China imepiga hatua na kuwa mtoaji mkubwa wa ufadhili wa masomo kwa wanafunzi kutoka nchi zinazostawai, ijapokuwa si rahisi kukokotoa mtiririko wake.

## LENGO LA 4.C. WALIMU

Sehemu ya walimu wenye kiwango cha chini cha kuhitimu kinachohitajika imekuwa ikipungua duniani kote. Katika kiwango cha elimu ya msingi, sehemu hiyo imepungua kutoka asilimia 90 katika mwaka 2010 hadi asilimia 85 katika mwaka wa 2023, huku jumla ya walimu ikiongezeka kwa zaidi ya milioni tano. Barani Ulaya na Amerika Kaskazini, sehemu wa walimu walio na kiwango cha chini cha kuhitimu ilipungua kutoka asilimia 98 katika mwaka wa 2010 hadi asilimia 93 katika mwaka wa 2023.

Ukosefu wa walimu wa kutosha ni tatizo la kote duniani, lakini unatokana a vyanzo viwili tofauti: uhaba wa walimu (ukosefu wa watafutakazi waliohitimu wa kutosha) au ukosefu wa nafasi za kazi za kutosha za walimu. Changamoto hizi mbili mara nyingi huunganishwa kwa sababu zinaleta matokeo sawa, kama vile uwiano wa juu kati ya wanafunzi na walimu, sehemu kubwa ya walimu ambao hawajahitimu au hawajapata mafunzo, kiwango cha juu cha kufunza 'nje ya ujuzi' (yaani somo ambalo halihusiani na utaalamu wa mwalimu), zamu mbili na madarasa ya zaidi ya gredi moja. Uhaba wa walimu katika nchi tajiri sanasana unatoka na upande wa mgao, huku vijana wakiwa na shauku ndogo katika taaluma hii na kupungua kwa usajili katika mipango ya kutayarisha walimu. Nchini Australia, idadi ya wanaohitimu kutoka mafunzo ya mwanzo ya walimu imepungua kwa asilimia 17 kati ya 2017 na 2020, na mfululizo wa mageuzo, ikiwa ni pamoja na ufadhili wa masomo ya walimu, yameletwa. Kinyume chake, katika baadhi ya nchi maskini, idadi ya watafutakazi za ualimu waliohitimu inapita idadi ya nafas za kazi za ualimu zinazopatikana. Nchini Senegal, ambapo kama asilimia 25 ya walimu hawana kiwango cha chini cha kuhitimu kinachohitajika, serikali iliajiri watafutakazi 2,000 kati ya 3,000 waliofaulu katika shindano la kuwa walimu katika mwaka wa 2020.

Mafunzo ya kazini ni kigezo muhimu katika kudumisha walimu kazini, ilhali ni asilimia 45 tu ya nchi zina sera inayofanya maendeleo ya kitaaluma ya mara kwa mara kuwa sharti katika elimu ya chekechea; asilimia 53 zina sera kama hiyo kwa ajili ya elimu ya msingi na sekondari. Nchi zilizostawi zaidi zina uwezekano mkubwa zaidi wa kuhitaji kiwango cha juu zaidi cha kuhitimu kimasomo kwa walimu na wa kufanya maendeleo ya kitaaluma kuwa lazima.

## FEDHA

Katika mwaka wa 2022, matumizi katika elimu duniani kote, yanayojumuisha michango ya serikali, wafadhili na kaya, yaliongezeka kwa asilimia 0.8 kufikia Dola trilioni 5.8 za Marekani, licha ya kupungua kwa matumizi ya serikali kutoka Dola trilioni 4.39 hadi Dola trilioni 4.33. Duniani, matumizi ya serikali katika elimu yalipungua kwa pointi 0.4 za asilimia ya Pato la Taifa kati ya 2015 na 2022: kiwango cha kati kilipungua kutoka asilimia 4.4 hadi asilimia 4 na wastani ulipungua kutoka asilimia 4.6 hadi asilimia 4.3. Tukichukua kiwango cha kati kama kipimo, matumizi ya serikali katika elimu yameongezeka sana katika nchi zenye mapato ya chini kutoka asilimia 2.6 katika mwaka wa 2010 hadi asilimia 3.2 katika mwaka wa 2015 na asilimia 3.8 katika mwaka wa 2022. Kinyume chake, kiwango hicho


kilipungua kutoka asilimia 4.5 katika mwaka wa 2013 hadi asilimia 3.5 katika mwaka wa 2021 katika nchi zilizo kwenye kiwango cha chini miongoni mwa nchi zenye mapato ya wastani.

Jumla ya matumizi ya serikali kama sehemu ya Pata la Taifa ni zao la viashiria viwili: jumla ya matumizi ya serikali na kipaumbele ambacho serikali zinawekea bajeti zao za elimu. Hicho cha mwisho kilipungua kwa pointi 0.6 za asilimia kutoka asilimia 13.2 katika mwaka wa 2015 hadi asilimia

**MCHORO WA 9:**

**Idadi ya fedha inayotumika katika elimu ya umma duniani imepungua kidogo tangu mwaka wa 2015**

*a. Matumizi ya serikali katika elimu ya umma kama sehemu ya Pato la Taifa, kulingana na kundi la mapato ya nchi, 2010–2022*




*b. Sehemu ya elimu katika matumizi ya jumla ya serikali, kulingana na kundi la mapato la nchi, 2010–2022*




*GEM StatLink:* https://bit.ly/GEM2024_Summary_fig9
Chanzo: Hifadhitada ya EFW

12.6 katika mwaka wa 2022, yaani kwa zaidi ya punguko la matumizi ya jumla ya serikali katika elimu kama sehemu ya Pato la Taifa. Sehemu ya elimu katika jumla ya matumizi ya serikali katika nchi zenye mapato ya chini iliongezeka kutoka asilimia 13.2 katika mwaka wa 2015 hadi asilimia 15.6 katika mwaka wa 2022 lakini ilipungua sana kutoka asilimia 17.1 katika mwaka wa 2011 hadi asilimia 13.8 katika mwaka wa 2022 katika nchi zilizo kwenye kiwango cha chini miongoni mwa nchi zenye mapato ya wastani, hali ambayo huenda ni athari ya tatizo la ongezeko la madeni (**Mchoro wa 9**) . Kuhusiana na vigezo pacha vya kimataifa vya kutumia angalau asilimia 4 ya Pato la Taifa na angalau asilimia 15 ya matumizi ya serikali katika elimu, nchi 59 kati ya 171 hazikutimiza kigezo chochote kati ya hivyo viwili, ilhali nchi 34 zilitimiza vyote viwili.

Katika muktadha wa msukumo wa kila wakati wa mahitaji mengi kwenye bajeti za elimu, inazidi kuwa vigumu kulipa vizuri ili kuwavutia watu wenye vipaji kuwa wakuu wa shule. Hata hivyo, nchi chache, ikiwemo Italia (ambayo tayari ilikuwa na viwango vya juu) na Latvia (ambayo ilikuwa na viwango vya chini) zimeongeza pakubwa mishahara ya wakuu wa shule katika miaka michache iliyopita. Italia ilianzisha mageuzi ya uhuru wa uongozi wa shule, hali ambayo iliimarisha sana mishahara ya wakuu wa shule.

Jumla ya misaada kwa elimu ilifikia kiwango cha juu zaidi cha Dola bilioni 16.6 za Marekani katika mwaka wa 2022, ikiongezeka kwa Dola bilioni 14.3 katika mwaka wa 2021, ongezeko halisi la asilimia 16 kati ya miaka hiyo miwili. Licha ya ongezeko la jumla la ufadhili wa elimu, sehemu ya elimu katika jumla ya ODA, ambaup iliongezeka kutoka asilimia 8.2 katika mwaka wa 2013 hadi asilimia 9.3 katika mwaka wa 2019, imepungua, ikifikia asilimia 7.6 katika mwaka wa 2022. Ufadhili wa miradi ya tabianchi, chanzo ambacho huenda ni muhimu sana katika kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, haujatumika hata kidogo katika elimu.

Kaya huchangia kama robo ya matumizi ya elimu duniani, sehemu ambayo imeongezeka kidogo katika miaka ya hivi majuzi. Kaya zilitengea elimu kiwango cha kati cha asilimia 2.9 ya bajeti za kaya katika nchi zilizo kwenye kiwango cha chini miongoni mwa nchi zenye mapato ya wastani, ikilinganishwa na asilimia 1.3 katika nchi zenye mapato ya juu. Katika baadhi ya nchi, kama vile India, matumizi ya kaya zote katika elimu yaliongezeka kutoka asilimia 2.1 hadi asilimia 2.8 ya Pato la Taifa kati ya 2010 na 2021, huku katika baadhi kama vile Kenya, yalipungua kutoka asilimia 4.3 hadi asilimia tatu katika kipindi hicho hicho. Tofauti za kieneo ni kubwa sana; kwa mfano, kaya nchini Namibia hutumia fedha mara sita zaidi ya zilizo Senegal.

# Uongozi katika elimu

## ONGOZA KWA AJILI YA ELIMU

Viongozi wa elimu huelekeza timu, asasi na nchi zao. Hakuna njia moja tu ya kuongoza, hali inayofanya iwe vigumu kutathmini athari ya kiongozi. Hata hivyo, viongozi bora wa shule, wa mifumo na wa kisiasa wanahitajika sana kuelekeza elimu ipasavyo, kwa sababu changamoto ni kubwa.

Dhana ya viongozi wa shule imekuwa tofauti katika nchi mbalimbali kwa muda. Nafasi ya kutekeleza wajibu na kufanya maamuzi, muktadha wa kazi na usuli wa mtu binafsi huathiri vitendo vya kiongozi. Isitoshe, inazidi kutambuliwa kwamba kuna haja ya kuacha kuzingatia sana majukumu ya utawala na usimamizi na badala yake kuzingatia matokeo ya elimu, kama vile ujumuifu katika elimu na ustawi.

*Ripoti ya Dunia ya Ufuatiliaji wa Elimu ya 2024/2025* inatathmini hatua zilizopigwa kuelekea malengo ya 2030 na inaonyesha kwamba, ijapokuwa watoto wengi zaidi wako shuleni na wanamaliza elimu ya sekondari kuliko wakati mwingine wowote ule, hakukuwa na maendeleo katika baadhi ya vigezo. Uongozi ni muhimu sana katika kukabiliana na hali hii. Hakuna shule zinazoboresha matokeo ya wanafunzi bila kiongozi bora kuonyesha njia. Kwa msingi wa uchambuzi wa sheria na sera kuhusu kuajiri, matayarisho na mazingira ya kazi ya wakuu wa shule katika mifumo 211 ya elimu, ripoti hii inajadili nguvu za sera za kuvutia na kudumisha viongozi wenye vipaji.

Uongozi haupatikani tu katika viongozi wa shule: unapatikana pia kwa watu wenye nyadhifa zingine ndani na nje ya mfumo wa elimu, kuanzia manaibu wakuu wa shule, walimu na wanafunzi, uongozi unaposhirikiwa, viongozi wa kisiasa, asasi za raia, mashirika ya kimataifa, vyama na vyombo vya habari, ambao wanasaidia kubainisha malengo ya elimu.

Ripoti hii inatoa wito wa kukuza viongozi katika vipengele vinne muhimu vya uongozi ili waweze ***kubainisha matarajio, kuzingatia ujifunzaji, kukuza ushirikiano na kuendeleza watu***. Ili vipengele hivi vitimizwe, watu walio katika nafasi za uongozi wanastahili kuaminiwa na kuwezeshwa, kuajiriwa kupitia michakato yenye usawa, kusaidiwa kukua na kuhimizwa wakuze utamaduni wa ushirikiano. Ripoti hii pia inatoa wito wa kuwekeza katika kukuza uwezo wa maafisa wa elimu kuhudumu kama viongozi wa mifumo huku ikisisitiza sana uongozi elekezi na uhakikishaji wa ubora.

unesco
Global Education Monitoring Report

Sustainable Development Goals

www.unesco.org/publications ▪ www.unesco.org/gem-report